

MADA

UCHAMBUZI WA TAMATHALI ZA USEMI PAMOJA NA MBINU
NYINGINE ZA MATUMIZI YA LUGHA KATIKA UTENZI WA
MIKIDADI NA MAYASA

NA

OMAR SAID MOHAMMED

NAMBARI YA USAJILI: C50/66131/2010

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA
MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A.) KATIKA CHUO KIKUU
CHA NAIROBI

IDARA YA ISIMU NA LUGHA

CHUO KIKUU CHA NAIROBI

2012

i

University of NAIROBI Library



0389186 8

IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.



31/10/12

OMAR SAID MOHAMMED

TAREHE

(MWANAFUNZI)

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi walioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.



31/10/12

PROF. KINEENE WA MUTISO

TAREHE

(MSIMAMIZI)



31.10.2012

MWALIMU BASILIO, G. MUNGANIA

TAREHE

(MSIMAMIZI)

TABARUKU

Kazi hii namtabarukia shemeji yangu na ndugu yangu anayenipenda na kunijali Mbarak Abdulqadir Abdallah aliyenitia ari ili nijiendeleze kimasomo. Nawatabarukia pia marehemu nyanya yangu Fatma Abdallah Abulrahmani, marehemu baba yangu pamoja na mama yangu aliye hai kwa wakati huu niloandika tasnifu hii. Kadhalika namtabarukia mke wangu mpendwa Bi Warda Alwy Mohamed, aliye pia mwalimu mwenzangu kwa juhudi zake na uvumilivu wake tukiwa tu pamoja masomoni na bila ya kumsahau shemeji yangu aliye pia binamu yangu anayenipenda Bi Zakia Alwy Mohamed na mume wake mpendwa Bwana Ali Bakari Muhammad paomja na ndugu zangu wote.

SHUKRANI

Kwa jina la Mwenyezi Mungu muweza wa kila jambo naanza kwa kumshukuru yeye kwa kunijaalia mimi kuwa hapa ulimwenguni na kunilinda hadi wakati huu. Kazi hii haikuwa ni kwa kupitia bidii yangu peke yake bali kuna msururu w wapendwa wangu ambao wamechangia katika ufanifu huu.

Natoa shukrani zangu za dhati kwa wasimamizi wangu Prof. Kineene Wa Mutiso pamoja na Mwalimu Basilio Gichobi Mungania kwa ushauri wao ambao wamechangia katika kuniwezesha kufanya kazi hii.

Shukrani zingine ziwaendee walimu wangu katika Idara ya Isimu na Lugha, Chuo Kikuu cha Nairobi kwa mafunzo yao na mchango wao mkubwa na ulio maridhawa. Miongoni mwao ni : Prof. Kineene Wa Mutiso, Mwalimu Basilio Gichobi Mungania, Dkt. Iribe Mwangi, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Zaja Omboga, Dkt. Mbuthia Mwangi, Dkt. Raya Timammy, Dkt. Mwenda Mbatiah, Prof. John Habwe na Dkt. Amir Swaleh. Aidha namshukuru tena Prof. Kineene Wa Mutiso kwa kunihimiza kuendelea tena na safari hii endapo nitakamilisha shahada hii ya uzamili. Namshukuru pia Dkt. T. M. Olali kwa ushauri wake alionipatia siku iliyokuwa nilipowasilisha sura ya kwanza ya tasnifu hii mbele ya wataalamu wanajopo wa Chuo Kikuu cha Nairobi. Maoni yake yaliweza kuwa mwongozo wa kutegemewa kwangu.

Shukrani zangu pia ziwaendee wanafunzi wenzangu tuloanza pamoja safari hii muhimu. Tulizoeana sana na wao na kusaidiana kwa hali na mali, kwa msiba na kwa furaha. Wao ni Grace Mjomba, Gatakaa G, Manoti, Nixon Migiro, Otwere, Rono,

Kavivi Jackline, Janet Mwendu, Naliaka, Onchangu Rael, Mswenje, Monica Ruto, Ogola Benard, Ndege, Obure, Modgen Chisia, Maina Kenguro, Bore David, Doreen, Jenifer, Kiunga na Florence.

Shukrani za zaidi ni kwa mke wangu mpendwa Warda Alwy Mohamed aliyekuwa karibu nami na kunifaa kwa hali na mali. Shukrani kwa msaada wako wa kifedha na kujitolea kwako kuona kwamba lengo nililolilenga limefaulu. Asante kwa kuhakikisha kwamba nimeweza kupata tarakilishi ambayo imenifaa sana katika utafiti wangu. Licha ya kwamba naye pia alikuwa anasoma alihakikisha kwamba amenipatia mimi kipau mbele kwanza kwa kuhakikisha nimelipa ada ya chuo kwa wakati. Asante pia kwa wale wote waliopata kunijua kwa maombi yenu.

Asante kwa wale wliokubali kuhojiwa nami kama vile Ustadh Mahmoud Abdulqadir (Mau), miongoni mwa wengine bila kumsahau Mwalimu Mkuu wa shule ninayofunza Bwana Njuguna P. M. kwa kunijali na kunihimiza. Nakumbuka nilipokuwa ninakuomba ruhusa kuja Nairobi ukiniambia “Siwezi kumkatalia mtu ruhusa ambaye anataka kujikuza kiakademia”

Mwisho siwezi kuwasahau watoto wangu Haifat, Nagib na Fatma ambapo wao hawakuacha kuniswali kila nilipokuwa nikidurusu na kufanya kazi zangu za chuo kikuu. Miongoni mwa maswali yao ni: “Kwani mwalimu husoma kama mwanafunzi?”

“Baba mbona wewe wafanya *home work*?” “Baba mwalimu wako ni nani?” Haya na maswali mengine mengi waliweza kuniuliza kila wakati. Hata hivyo sikuwa nikiwadanganya bali niliwapatia majibu sahihi lakini kwa sababu ya umri wao mdogo hawakuweza kung’amua nilichokuwa nikiwajibu.

MUHTASARI

Utafiti huu unahusu uchambuzi wa tamathali za usemi na mbinu nyengine za matumizi ya lugha katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa* na Said Abdalla Masudi el Buhry el Hinawy.

Kazi hii imegawanywa katika sura nne. Katika sura ya kwanza tumeelezea swala letu la utafiti, madhumuni ya utafiti na nadharia tete zinazotuongoza. Isitoshe tumeeleza sababu za kuchagua mada hii pamoja na kufafanua upeo na mipaka ya somo hili, yaani utafiti wetu. Pia tumefafanua msingi wa kinadharia wa utafiti pamoja na yaliyoandikwa kuhusu somo hili, mbinu za utafiti na uchanganuzi wa data.

Katika sura ya pili tulitanguliza kwa kueleza maana ya fani pamoja na kuvitolea maelezo vipengele mbalimbali vya fani kikiwemo kipengele cha tamathali za usemi na mbinu nyingine za matumizi ya lugha. Tumewarejelea wataalamu mbalimbali katika kurejelea vipengele hivyo.

Sura ya tatu tumebainisha tamathali tofauti tofauti za usemi pamoja nambinu nyingine za matumizi ya lugha zilizotumika katika utenzi huu na kuzitolea maelezo yake. Sura ya nne ni hitimisho. Tumeeleza tuliyoyatambua na kutoa mapendekezo ya utafiti zaidi.

YALIYOMO

Mada	i
Ikirari.....	ii
Tabaruku	iii
Shukrani	iv
Muhtasari	vi
Yaliyomo	vii

SURA YA KWANZA.....	1
1.0 Utangulizi	1
1.1 Tatizo la utafiti.....	6
1.2 Madhumuni ya utafiti	7
1.3 Nadharia tete	7
1.4 Sababu za kuchagua mada hii.....	8
1.5 Upeo na mipaka ya Somo	9
1.6 Msingi wa kinadharia wa Utafiti	10
1.7 Yaliyoandikwa kuhusu somo hili	14

1.8 Mbinu za utafiti	17
1.8.0 Utangulizi	17
1.8.1 Mbinu za ukusanyaji data	17
1.8.2 Uchanganuzi wa data	17
1.9 Hitimisho	18
SURA YA PILI	19
2.0 Utangulizi	19
2.1 Dhana ya fani.....	19 ⁵
2.2 Lugha	21
2.3 Uhuru wa kishairi	24
2.3.1 Msamiati wa ushairi	25
2.4 Wahusika	27
2.5 Mandhari	29
2.6 Toni	30
2.7 Muundo	31
2.8 Mtindo	32
2.9 Tamathali za usemi	34

2.9.1 Tashbihi	35
2.9.1.1 Sítíari	36
2.9.1.2 Maswali ya balagha	36
2.9.1.3 Kejeli	37
2.9.1.4 Chuku	37
2.9.1.5 Tashihisi	37
2.9.1.6 Dhihaka	38
2.9.1.7 Lakabu	38
2.9.1.8 Majazi	38
2.9.2 Mbinu nyengine za matumizi ya lugha.....	38
2.9.2.1 Tabdila	38
2.9.2.2 Inkisari	39
2.9.2.3 Mazida	40
2.9.2.4 Takriri.....	40
2.9.2.5 Ukiushi wa kisarufi	41
2.9.2.6 Taswira	41
2.9.2.7 Misemo	42

2.9.2.8	Usambamba	42
2.9.2.9	Visawe	42
2.9.2.10	Mbinu rejeshi	43
2.9.2.11	Utohozi	43
2.9.2.12	Taharuki	43
2.9.2.13	Nahau	43
2.9.2.14	Hitimisho	44
 SURA YA TATU		45
3.0	Tamathali za usemi	45
3.1.0	Tashbihi	45
3.1.1	Sitiari	46
3.1.2	Maswali ya balagha	48
3.1.3.	Kejeli	49
3.1.4	Chuku.....	51
3.1.5	Tashihisi	52
3.1.6	Dhihakaka	53

3.1.7 Lakabu	54
3.1.8 Majazi	55
3.2.0 Mbinu nyingine za matumizi ya lugha.....	57
3.2.1 Tabdila	57
3.2.2 Inkisari.....	58
3.2.3 Mazida.....	59
3.2.4 Takriri	60
3.2.5 Ukiushi wa kisarufi	62 ⁴
3.2.6 Taswira	63
3.2.7 Misemo	65
3.2.8 Usambamba	65
3.2.9 Visawe	66
3.2.10 Mbinu rejeshi.....	67
3.2.11 Utohozi	70
3.1.12 Taharuki	71
3.1.13 Nahau.....	72
3.2.14 Hitimisho.....	74

SURA YA NNE	75
4.0 Hitimisho.....	75
Utangulizi	75
4.1 Muhtasari wa maswala muhimu.....	75
4.2 Kuhusu nadharia tete	77
4.3 Mapendekezo	77
Tuliowahoji	78
Marejeleo	79 ^t

ALAMA ZILIZOTUMIKA

1. T.U.K.I.- Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.
2. k.m.- Kwa mfano.
3. uk.- Ukurasa.
4. k.v.- Kama vile.
5. ub.- Ubeti

SURA YA KWANZA

1.0 UTANGULIZI

Fasihi ni sanaa inayotumia lugha kama mali ghafi yake. Imegawika katika matawi mawili makuu : andishi na simulizi. Matawi haya yana tanzu zake, nasi tutajikita katika utanzu wa ushairi wa fasihi andishi. Utafiti wetu utahusu moja katika bahari za ushairi ambao ni utenzi au utendi kama wataalamu wengine wanavyouita. Sisi tutashughulikia uchambuzi wa tamathali za usemi na mbinu nyingine za matumizi ya lugha katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*. Tutaelezea japo kwa muhtasari yali yanayohusiana na utenzi huu. Mada ya utenzi ni Mikidadi na Mayasa. Maneno hayo mawili ni miongoni mwa majina ya wahusika katika utenzi huu. Majina ya wahusika hawa yametumika kimajazi na yametokana na lugha ya Kiarabu. Mikidadi ikimaanisha kitu au kifaa kinachokata nalo jina la Mayasa lina maana ya mwanamke mwenye maringo. Maelezo haya tuliyapata kupitia mahojiano baina yetu na Ustadh Mahmoud Abdulqadir Mau, Mwanachuoni kutoka mjini Lamu.

Utenzi huu unahusu kisa cha mashujaa hawa wawili waliotaka kuoana lakini wakawekewa pingamizi ili wasiowane. Mayasa alikuja kuposwa na wanaume wengi na hakuna hata mmoja wao aliyeafikiwa kumpata kwa vile hawakuweza kutekeleza yale masharti yake kwamba mwenye kumuoa yeye sharti apigane naye na amshinde. Mikidadi akafanya hivyo na akamshinda Mayasa na hata akaweza kumvua taji lake. Jabiri, babake Mayasa, akaweka pingamizi kwa vile hakutaka binti yake aolewe na mtu maskini. Aliwaita ndugu zake kwa lengo la kufanya mashauri na ikaamuliwa Mikidadi awekewe kiwango kikubwa cha mahari asichoweza

kukitimiza lakini Mikidadi akakubali. Alipewa muda wa miezi mitatu awe ashaleta mahari na akatimiza ahadi hiyo.

Mikidadi kurudi mjini kwao tu akapashwa habari kuwa Mayasa anaolewa na Maliki Bin Riyahi. Mikidadi akapigana na jeshi lililokuwa likimlinda Mayasa na kulishinda. Mwishowe wawili hawa wakaoana.

Utenzi ni miongoni mwa bahari za ushairi ambao ni mkongwe sana. Njogu na Chimera, (1999:10) wanadai kwamba, kufikia sasa, ithibati zilizopo zinaonyesha kuwa huenda *Utenzi wa Tambuka* ndio utungo wa kwanza kuandikwa katika lugha ya Kiswahili. Uliandikwa na Mwengo bin Athmani mnamo mwaka wa 1728. Wanaendelea kudai kuwa tungo zilizokuwepo kabla ya hapo zilikuwa zikisimuliwa na kusambazwa kwa mdomo.

Utendi ni utungo ambao huandikwa ama kukaririwa au kuimbwa kwa lugha ya kisanaa iliyo teule na ya mkato, ili kupitisha ujumbe au maudhui kutokana na tajriba ya mwanasanaa husika. Ujumbe unaopitishwa huwa ni mzito na unaweza kuwa wa kihistoria, kidini na hata maelezo kuhusu mtu fulani kwa mapana. Huwa na kina kimoja katika kila mshororo na idadi maalum ya mizani.

Wamitila (2003:334) anadai kuwa utenzi ni istilahi inayotumiwa kuelezea utungo unaosimulia kitu fulani kwa mapana. Kimuundo, utendi huwa na kina kimoja cha nje au kina cha utao. Aghalabu kina cha mwisho cha kila ubeti hurudiwa. Anaendelea kusema kwamba hapana idadi maalum ya mizani katika kila mshororo.

Kauli hii ya kuwa hapana idadi maalum ya mizani katika kila mshororo yamedhihirika katika utenzi ufuatao:

/Bi /smi/ lla/ hi/ na/i/ ka /di/mu/	mizani 9
/ha/li/ya/ku/tu/nga/hi/no/nu/dhu/mu/	mizani 11
/Na/ar/Rah/ma/ni/ki/i/ra/si/mu/	mizani 10
/ba/si/ar/Ra/hi/mi/nyu/ma/i/ka/ye/	mizani 11

(ubeti wa 1 *Al-Inkishafi*)

Mbatiah (2001:106) asema kwamba utenzi ni aina ya ushairi unaojipambanua kwa urefu wake na uzito wake wa maswala unayoyashughulikia. Utendi huwa ni mseto wa masimulizi na maelezo yenye urefu wa mamia au maelfu ya beti, juu ya wahusika, tukio au jambo zito. Anaendelea kusema kuwa mtindo wake pia huwa wa hadhi ya juu.

Njogu na Chimera (1999:102) wanasema utenzi ni ushairi wenye mizani chache kuliko kumi na mbili, na ambao mara nyingi hauna vina vya kati katika mishororo, bali kila ubeti una vina vya namna moja katika mistari yake; isipokuwa mistari wa mwisho katika kila ubeti. Kina hicho kinachorudiwarudiwa katika kila ubeti wa utenzi chaitwa bahari. Abedi (1954:29) anasema, utendi ni ushairi wenye mizani chache kuliko kumi na mbili, ambao mara nyingi hauna vina vya kati katika mistari, bali kila ubeti una vina vya namna moja katika mistari yake isipokuwa mistari wa mwisho katika kila ubeti, ambao huendelea na kina cha namna moja kinachoitwa bahari. Maoni ya wataalamu hawa yako sawa.

Utenzi una sifa ya urefu miongoni mwa sifa nyengine. Huku ni kusema kwamba, utungo huu hutumiwa kusimulia visa au maudhui marefu yanayohusiana na maswala yanayomkumba binadamu katika tajriba zake ulimwenguni. Utendi yamkini uwe ni juu ya maisha na matendo ya mashujaa wa dini kama vile Mtume Muhammad (S.A.W) wa Waislamu na Masihi Issa wa Wakristo na Waislamu. Tendi zaweza kutaja juu ya maisha na matendo ya mashujaa na wababe wa kitamaduni wa jamii fulani kama vile Fumo Liyongo wa Waswahili, Luwanda Magere wa Wajaluo, Syokimau wa Wakamba, Lenana wa Wamaasai miongoni mwa wengine. Pia kuna tenzi zinazozungumzia maswala ya dini, mapenzi na wosia.

Mifano ya tenzi za kidini ni *Al- Inkishafi*, *Kiokozi cha Banati* na *Kasida ya Hamziya*. Utenzi wa mahaba ni pamoja na *Mwana Nazi*, *Mwana Ninga* na nyinginezo. Mfano wa utenzi wa wosia ni *Utenzi wa Mwana Kupona* ambao unahusu wosia wa mzazi kwa mwanawe wa kike. *Utenzi wa Siraji* ambao ni utendi wa Mohamed Kijumwa alioutunga kwa lengo la kumpa mwanawe Helewa mawaidha.

Tukigusia historia ya ushairi japo kwa muhtasari, baadhi ya maswali ya kujiuliza ni kama: Ushairi wa Kiswahili ulianza lini? Ni utungo upi unaoweza kudaiwa kuwa ndio wa kwanza katika fasihi ya Kiswahili miongoni mwa maswala mengine. Wamitila (2002:95) anasema kuwa licha ya kuwoko kwa maandishi mengi, suala hili linakuwa na ugumu wa kukatiwa kauli. Ili kuthibitisha kauli hii kuwa upo ugumu wa kuamua ni upi utungo wa kwanza, tuangalie maoni ya wanavyuoni hawa.

Wamitila (2002:95) anasema kuwa: kwa mujibu wa wahakiki wengi utungo wa kwanza wa kishairi ni Hamziya. Huu ni utungo wa kikasida unaomsifu mtume Muhammad

(S.A.W). Utungo huu unasemekana ulitungwa mwaka wa1652 BK au hata kabla na ni tafsiri ya utungo wa Kiarabu '*Ummu ul Qura*' (*Mama wa Miji*) wa mshairi wa Kisufii kutoka Misri. Njogu na Chimera (1999:104) wanasema kuwa utungo wa Hamziya ulitungwa mwaka 1749 na Sharif Aidarus bin Uthman. Tukiangalia maoni ya wataalamu hawa tunapata ile ithibati ya kwamba hakuna anayejua hakika ni utungo gani ndio wa kwanza kwa maana wote hawa watatu wametoa tarehe tofauti kuhusu utungo huo huo mmoja.

Hata hivyo, tenzi zinabaki tu kuwa tungo kongwe kama tulivyotaja hapo awali. Miongoni mwa tenzi kongwe za Kiswahili, ni pamoja na *Utenzi wa Siri Li Asirari*. Utenzi huu ulitungwa na Binti Bwana Lemba Mwana Mwarabu, mwaka 1663 na una beti 563 (Wa Mutiso, 1996:57). Kuna *Utendi wa Mwana Fatuma* uliotungwa mwaka wa 1807 na Mwana (Mwenye) Said (Sayyid) Amin bin Said Uthman Al- Mahdalay na una beti 446 (Wa mutiso 1996:61). Nao *Utenzi wa Rasi'l Ghuli* uliotungwa mwaka wa 1850 na Mgeni bin Faqihi na una beti 4584. Utendi huu unadaiwa kuwa ndio mrefu kuliko zote zilizopata kuchapishwa katika lugha yoyote ile ya Kiafrika, na unasemekana ni wa pili kwa urefu miongoni mwa tenzi za Kiswahili zinazojulikana (Kessel 1997:V).

Utendi wa Fumo Liyongo uliotungwa na Muhammad Kijumwa na *Utendi wa Sifa za Mwana Munga/ Utendi wa Mwana Munga* (unaodaiwa kuwa ulitungwa na Fumo Liyongo) ndio unaodaiwa kuwa ndio utenzi wa kale zaidi sana uliotungwa mwaka wa 1517 kulingana na (Wamitila 2002:95).

Mtunzi wa tenzi hutumia mbinu mbalimbali za lugha, mbinu ambazo bila shaka zinaweza kuchanganuliwa. Mbinu hizi za lugha zina nafasi kubwa na muhimu katika

uchanganuzi wa matini au kazi za kifasihi zikiwemo tenzi. Ingawa utendi huu wa Mikidadi na Mayasa ni miongoni mwa tenzi kongwe, wataalamu na watafiti wa fasihi hawajaufanyia utafiti mwingi jinsi vile walivyozifanyia tenzi nyingine. Kwa maoni yetu, tunaona ni vyema tuupe utenzi huu kipaumbele ili usije ukasahaulika. Tuna imani thabiti kwamba utenzi huu kama zilivyo tenzi nyingine za Kiswahili, umesheheni mawazo muhimu yanayohusu matukio mazito. Kwa hivyo, lau uchanganuzi kama huo tuliodhamiria usipofanyika, itabaki kuwa vigumu kwa walengwa ama hadhira kuusoma na kupata mawazo au maudhui yake kwa kina. Ikiwa basi hatutatimiza lengo hili, utungo huu maarufu ambao una mchango mkubwa katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili, tutakuwa hatukuutendea haki inayostahili.

1.1 TATIZO LA UTAFITI

Wengi wa wataalamu waliotangulia walioshughulikia kazi za tenzi tulibaini kuwa waliwacha pengo fulani katika kazi zao. Kina Harries (1962), Knappert (1979), na Mulokozi (1999), ni miongoni mwa maulamaa walioshughulikia tendi za jadi. Katika kazi zao hizo walijikita ama katika tarjumi au uhakiki wa kimaudhui.

Kilichotupelekea sisi kushughulikia kufanya uchambuzi wa tamathali za semi na mbinu nyingine za matumizi ya lugha katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* ni kwamba hakuna aliyewahi kushughulikia vipengele hivi vichache tu vya fani katika utenzi huu bali walishughulikia uhakiki wa fani kwa jumla na walijumuisha tenzi mbili na nadharia waliotumia wao ni tifaute na yetu.

Mungai (2005) alishughulikia ulinganishi wa kifani wa tenzi mbili, *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* na *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa* wakitumia nadharia ya urasimu. Utafiti wetu unapania kuchambua vipengele hivi vya fani kwa undani zaidi, kuona jinsi vilivyojengeka na jinsi vinavyotumika ili kuwasilisha maana katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*.

1.2 MADHUMUNI YA UTAFITI

Lengo kuu la utafiti wetu ni kuhusu uchambuzi wa tamathali za usemi na mbinu nyingine za matumizi ya lugha katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*. Utafiti wetu umeshughulikia maswala yafuatayo:

- i) Kuchambua uteuzi wa tamathali za usemi na mbinu nyingine za matumizi ya lugha katika utendi huu.
- ii) Kubaini kuwa uteuzi pamoja na matumizi ya tamtamthali za usemi na mbinu nyingine za matumizi ya lugha katika utendi huu ama umechangia katika ufanifu au udhaifu wa kazi hii.

1.3 NADHARIA TETE.

Utafiti wetu umejikita katika nadharia tete zifuatazo:

- i) Uteuzi wa tamathali za usemi pamoja na mbinu nyingine za matumizi ya lugha katika utendi huu umetekelezwa kwa malengo maalum.

- ii) Uteuzi pamoja na matumizi ya tamathali za usemi pamoja na mbinu nyengine za matumizi ya lugha katika utenzi huu umechangia katika ama ufanifu au udhaifu wa kazi hii.

1.4 SABABU ZA KUCHAGUA MADA HII.

Sababu kuu ya kuchagua mada hii ni upungufu uliopo kuhusiana na utafiti uliofanywa kuhusu utenzi huu. Tulipopitia kazi ya Mungai (2005), kuhusu ulinganishi wa kifani katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* na *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*, tulipata kuwa kuna tofauti juu ya kile alichokishughulikia na kile tumekishughulikia. Mungai (2005) alishughulikia ulinganishi wa kifani katika tenzi mbili, *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali* na *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*, akitumia nadharia ya urasimu. Sisi twashughulikia *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa* peke yake na tunatumia nadharia ya umuundo. Kuna na wale walioshughulikia fani katika tenzi tofauti na huu utenzi wetu. Kadenge (1982) alishughulikia ukiushi wa kaida za lugha katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*.

Sababu nyingine ni kuchangia katika taaluma ya kiusomi. Matarajio yetu ni kwamba kazi hii itakuwa ni ya manufaa makubwa kwa wasomi na watumizi wa lugha ya Kiswahili. Pindi wahusika hawa watakapopata fursa ya kuipitia kazi yetu, itawajia bayana kwamba tenzi au ushairi kwa jumla ambao wengi huchelea kuusoma kwa madai ya urefu na kwamba nyingi yazo zimetumia msamiati wa Kiswahili kilichochakaa na kusheheni msamiati wa Kiarabu, wataweza kuuelewa kwa urahisi. Vilevile utenzi huu una sifa mahsusi kama zilivyo tenzi nyingine ama kazi yoyote ile ya kisanaa. Kwa hivyo, tumeonelea ipo haja ya kuuchunguza ili kuzibaini sifa hizo kwa manufaa ya wanajamii.

Aidha kuna baadhi wanaodhania kuwa utanzu huu wa utenzi umejikita kwa asilimia kubwa na maudhui ya kidini hususan dini ya Kiislamu na kwamba hakuna budi kutumiwa msamiati wa kidini.

1.5 UPEO NA MIPAKA YA SOMO

Katika utafiti wetu tutashughulikia uchambuzi wa tamathali za usemi pamoja na mbinu nyingine za matumizi ya lugha katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Tutaupitia utenzi huu kwa lengo la kutambua na kueleza kipengele hiki cha tamathali za usemi pamoja na mbinu nyingine za matumizi ya lugha ambavyo ni miongoni mwa vipengele vya fani. Azma yetu ni kutumia nadharia ya umuundo katika kazi yetu. Katika kushughulikia mada hii yetu inapobidi tutarejelea ama tenzi nyingine zilizotungwa na mtunzi yuyu huyu wa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* katika kufafanua mtindo wa tamathali za usemi pamoja na mbinu nyengine za matumizi ya lugha au tenzi nyengine za waandishi wengine kama vile *Utendi wa Fumo Liyongo* ulioandikwa na Mohamed Kijumwa, *Utendi wa Howani Mwana Howani na Utendi wa Mwanakukuwa* ulioandikwa na Zaynab Hamid Mohammed miongoni mwa nyengine. Mbali na tenzi, tutajumuisha pia na bahari nyingine za ushairi.

Tutatathmini michango na mawazo ya wataalamu mbalimbali kuhusu vipengele hivi vya fani na kutoa mchango wetu. Aidha, tutavitaja tu kwa muhtasari baadhi ya vipengele vingine vya fani kama vile wahusika, mtindo, ploti, mandhari na vinginevyo katika kazi hii yetu.

1.6 MSINGI WA KINADHARIA WA UTAFITI

Utafiti wetu utafanywa na utajikita katika nadharia ya umuundo. Nadharia hii inahusiana na isimu kwa kiasi kikubwa. Inahusishwa na wana – isimu wa shule ya Prague kati ya 1928 –1946, ambao walihusika na Urasimu wa Kirusi kabla ya kuanguka kwake. Miongoni mwao ni pamoja na Roman Jakobson, Trubetzkoy, Claude Levi – Strauss na Rene Wellek. Mwasisi wa nadharia hii ni Fredinand de Saussure, mwana isimu wa Ki – Swizi. Wana – isimu hawa waliathiriwa na mawazo ya wahakiki wa kirasimu wa nchi za Zeshi na pia mawazo ya Fredinand de Saussure kuhusu dhana za ‘langage’, ‘langue’ na ‘parole’. De Saussure alibaini kuwa dhana za ‘parole’ (matumizi lugha) na ile ya ‘langue’ (mfumo lugha) kwamba lugha ina taratibu zake ambazo zinafaa kufuatwa na msemaji wa lugha hiyo (utendaji lugha).

De Saussure anadai kuwa lugha inayojulikana na wazungumzaji ‘langage’ inaundwa kutokana na sheria na kanuni za lugha ‘langue’ pamoja na matumizi yake katika mazungumzo na maandishi ‘parole.’ Wanamiundo walitumia dhana hizi kuisitiza kuwa fasihi iangaliwe kama mfumo ambao una kanuni zake zinazohitajika kueleweka na kila msanii katika matumizi yake kwenye mawasiliano na hata kimuundo.

Kulingana na wana miundo, uelewaji wa mfumo wa kazi za kifasihi humlazimu msanii achunguze matumizi ya lugha katika maandishi au mazungumzo pamoja na vipashio vyake na uhusiano wa vipashio hivyo. Kwa kusema hivi wanamuundo wanamaanisha kuwa fasihi ni mfumo unaojisimamia ‘langue’ na mfumo wenyewe una kanuni zake na kwamba ni wajibu kanuni hizo kufuatwa. Kwa hivyo katika

kazi yetu ya kuchanganua *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa* itatulazimu tuchanagane lugha ilyotumika pamoja na kaida zake na tutatathmini ikiwa mtunzi alizitekeleza kaida hizo.

Dhana hizi za '*langue*' na '*parole*' zilishughulikia uhusiano wa ishara inayotumiwa katika lugha na kiashiriwa chake au ishara na kitajwa. De Saussure aliuona ulimwengu wa lugha uliojengwa kwa viashiria na viashiriwa, na kuwa viashiriwa hubainishwa na viashiria. Wanaumuundo walidai kuwa maneno yanahusiana kwa namna mbili; kimlalo na kimuimo.

Mwari (2010:63) alisema kwamba, kulingana na de Saussure maneno katika sentensi huweza kuhusiana na mengine katika hali ya kiwima au kimlalo. Katika uhusiano wa kimlalo maneno huungana, hukubaliana na huingiliana katika matini hiyo na kuibua maana. Katika uhusiano wima fahiwa mbalimbali za maneno zaweza kutumiwa kurejelea neno moja katika matini na bado maneno hayo tofauti yakabeba maana moja; k.m. vitenzi vifuatavyo :

Alimpatia na alimkabidhi vina maana sawa na alimpa

Habwe na Karanja (2004:144) wanasema kwamba Saussure alieleza kuwa kila lugha ina mifumo tata, mifumo inayoingiliana, inayochukuana na kuendana. Ishara za kiisimu kulingana na Saussure, zilisimamia maana au dhana fulani. Kwa mujibu wa Saussure lugha ina vitu viwili, maana na ishara.

Mgullu (1999:8) anaeleza kuwa Saussure alionelea kuwa sauti za lugha ni nasibu na kwamba hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya kiashiria na kiashiriwa.

Pia aliona kuwa kuna kiashiriwa kimoja chenye viashiria tofauti tofauti katika lugha tofauti tofauti.

Kwa mfano:

Kiti- Kiswahili

Chair – Kiingereza

Giti- Kimeru

Ekerogo-Ekegusii

Kutokana na maelezo ya kwanza ya Saussure kwa mujibu wa Mgullu, tumepata kuona kwamba nadharia hii huweka mkazo mkubwa sana kwenye unasibishi wa maana. Maana hii nasibishi ni ile inayohusishwa na neno wala sicho kile kinachorejelewa, k.m. neno *simba*. Neno hili maana yake husishi ni mnyama wa pori ambaye kwa ule ujasiri wake anachukuliwa kama mfalme wa porini. Tukijikita katika maana nasibishi ya neno hili tutapata kwamba ni mtu ambaye ni jasiri sana asiyeshindika katika mambo mengi kama vile vita. Kwa wale wanaotumia nembo za wanyama k.v. *simba* na wengineo katika kampuni zao, mashirika hata vyama vya kisiasa, neno hilo *simba* linaweza kutumiwa kutoa maaana nasibishi nyingine pengine ya shirika fulani lenye sifa fulani nzuri kuliko mashirika mengine.

Kulingana na Saussure, kinachoathiri uelewa wetu wa vitu ni vile tunavyoitumia lugha katika kuvieleza vitu hivyo. Kwa mfano, hapo zamani miaka ya sabini hadi themaniini kabila la Kisomali lilipotajwa lilikuwa likinasibishwa na ubaya kama ilivyo sasa

jinsi vile wamagharibi wanavyochukulia kuwa wale Waarabu wanaojilipua kwa mabomu kuwa ni wabaya. Aidha watu hawa huko kwao wanaonekana kuwa wako sawa na ni wazalendo. Nadharia hii hutilia mkazo kwenye muundo wa kazi. Huku ni kumaanisha kwamba katika kazi yoyote ile mwandishi huwa hana nafasi. Hivyo basi nadharia hii itatufaa katika kushughulikia maswala ya fani ambapo tamathali za lugha ni moja wapo ya vipengele vya fani. Walichokichunguza wana-miundo ni muundo wa ndani wa kazi za kifasihi hususan za kishairi ndizo walizoshughulika nazo zaidi. Nadharia hii inasisitiza uhakiki wa kazi bila kuihusisha na jamii wala miktadha mengine yoyote k.v. ya kisiasa, kihistoria na kifilosofia. Pia ilipinga kuhusishwa kwa mwandishi.

Wana nadharia hii wanaangalia namna maneno yalivyopangwa na vile yalivyohusiana ili kutoa maana lakini isiyo na urejelezi wa nje na kwa hivyo inapuuza ufasiri wa msomaji. Kulingana na wao neno halihitaji urejelezi ili lipate maana. Umuundo humpuuza mwandishi katika uhakiki wake ili kufichua au kuweka wazi mifumo au harakati za kiuashiriaji ambazo zinatokea katika kazi hiyo. Wana-miundo wanaangalia maana ya kila neno katika sentensi na jinsi neno hilo lilivyohusiana na maneno jirani. Pia wanaangalia umbo la kazi za kifonolojia, kisintaksia, na kisemantiki. Kwa wahakiki wa ki-muundo, viashiria vina maana na uzito mkubwa kuliko viashiriwa.

Kwa vile nadharia hii inatilia mkazo muungano na mwingiliano wa vipengele mbalimbali vya kifani katika ujenzi wa umbo moja la kazi ya kifasihi basi itatufaa katika utafiti wetu na tuna imani kwamba tutafikia malengo yetu.

1.7 YALIYOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Historia ya tenzi ndiyo kongwe zaidi katika utanzu wa fasihi. Wataalamu wamesema kuwa tenzi zilikuwako hata kabla ya kufika kwa maandishi. Kulingana na Njogu na Chimera (1999:88) ushairi ulibuniwa kutokana na shughuli za kufanya kazi. Majilio ya wageni katika janibu hizi zetu za Afrika Mashariki wakiwemo Waarabu na Wazungu (Waingereza na Wajerumani) walikuja na hati zao. Huu ndio wakati kuliposhuhudiwa uandishi wa tenzi za Kiswahili kwa hati za Kiarabu na Kirumi. Kwa vile tenzi hizi ziliandikwa zamani sana, ilitarajiwa kuwa uhakiki wazo umeshugulikiwa kwa kina na maulamaa wa kifasihi.

Magwiji wa awali nchini Kenya ambao walikuwa ni wageni ndio waliozishughulikia kazi hizi, na nyingi yazo zilihusu ukusanyaji wa miswada kutoka kwa wenyeji, tarjumi na uhariri wa tenzi zilizopatikana. Miongoni mwa wataalamu hawa ni pamoja na Dammann, Jan Knappert, J.W.T. Allen, Lienhardt, Lambert na wengineo.

Ernst Dammann (1940) aligusia kwa uchache *Utenzi wa Mwana Fatumah* lakini kwa lugha ya Kijerumani. Kazi hii haina umuhimu mkubwa sana kwetu sisi kwa vile sisi si wazawa wa lugha hiyo na pia hatuimudu katika maandishi wala kimazungumzo. Ni imani yetu kwamba kwa wale wanaoimudu lugha hii bara bara basi kazi hii itakuwa ni tunu kubwa sana kwao. Uchunguzi wetu umedhihirisha kwamba wapo wataalamu walioshughulikia utendi huu wa Mikidadi na Mayasa, ila kile walichokishughulikia wao kilikuwa kina tofauti na chetu.

Mungai (2005) katika tasnifu yake ya M.A. alishughulikia uhakiki linganishi wa kifani wa tenzi mbili, *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* na ule *Utendi wa Swifa ya Nguvumali*. Tofauti iliyopo baina ya kazi yetu na ya Mungai ni kwamba mbali na yeye kushughulikia *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* pia alishughulikia na *Utendi wa Swifa ya Nguvumali* ilihali sisi tunashughulikia utendi mmoja tu *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Tofauti nyengine ni kwamba Mungai alishughulikia uhakiki wa fani nasi tunashughulikia uchambuzi wa tamathali za usemi pamoja na mbinu nyingine za matumizi ya lugha. Tamathali za usemi ni kipengele kimojawapo cha fani. Aidha nadharia aliyotumia Mungai ni urasimu ilihali yetu ni umuundo. Kuna tofauti baina ya nadharia hizi lakini si kubwa sana.

J.W.T. Allen (1971) naye aliutafsiri utendi huu kwa lugha ya Kiingereza naye Werner (1932) alifasiri beti mia moja na sitini za utendi huu ukikumbuka kwamba utenzi huu una beti 778. Wa Mutiso ameshughulikia kazi nyingi za ushairi. Ameshughulikia maudhui ya Hurafa na Uyakinifu katika *Kasida ya Hamziyya*. Alifasiri kasida hii kwa Kiingereza na kuihakiki pia katika *The Hamziyya Epic: Translation and Commentary*. Katika mwaka wa (1996) alihakiki *Kasida ya Burudai* katika tasnifu yake ya PhD. Aliitafsiri kasida hii kwa Kiingereza na kuifasiri kwa Kiswahili na ameihakiki kwa misingi ya “*Archetypal Motifs*”.

Wa Mutiso (2002) na (2003) alifasiri tenzi za Mwana Fatuma na Siri li Asirali mtawalia. Na (2005) alitafsiri *Kasida ya Hamziyya* na kuhakiki fani yake katika “Tarjumi maelezo na uhakiki.” Wa Mberia (1986) alihakiki *Utenzi wa Fumo Liyongo*.

Alimsifu Liyongo kama shujaa . Abdulaziz (1968) alishughulikia uchambuzi wa matumizi ya lugha katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*. Kadenge (1982) alishughulikia ukiushi wa lugha katika *Utenzi wa Swifa ya Nguvumali*. Tenzi za wawili hawa zimetupatia mwongozo katika kushughulikia mada yetu japo tenzi zenyewe hazifanani.

Mbayi (2009) naye alishughulikia uhakiki wa fani katika tenzi za *Howani Mwana Howani na Mwanakukua* za Zaynab Himid Mohammed. Kuna pia na wataalamu wa kigeni wa Kizungu walioshughulika na uhakiki wa tenzi za kale. Walishughulika na kuzikusanya tenzi hizi. Pia waliziandika kwa hati ya Kirumi na hata kuzihariri. Baadhi yao ni Harries (1962) ambaye alitafsiri na kuzihariri tenzi mbalimbali kwa Kiingereza zikiwemo tenzi za *Mwana kupona, Ras al Ghuli, Al – Inkishafi, Utendi Wa Hati, Utendi Wa Adili*, na *Utendi wa Liyongo*. Allan alishughulikia *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* kwa Kiingereza. Knappert (1964) alihariri *Utendi wa Yaqubu na Utendi wa Yusufu, Utenzi wa maisha ya Nabii Adamu, Utenzi wa Sayyidina Ali na Muhdhari bin Darimi*. Mwaka wa (1967) alifasiri *Utenzi wa Miraj* na *Tambuka* kwa Kiingereza.

Kazi zote hizi tulizozitaja ni rasilimali kubwa katika fasihi ya Kiswahili, na kama tulivyozungumza hapo awali ni kwamba tumekuwa tukizirejelea mara si haba hususan zile zilizoshughulikia vipengele vya fani.

1.8 MBINU ZA UTAFITI

1.8.0 Utangulizi

Utafiti unaweza kufanywa kwa kupitia njia au mbinu tofauti, kwa kutegemea ni aina gani ya utafiti unaoshughulika nao mtafiti. Kuna utafiti wa kufanyika katika maabara, maktabani, barabarani, nyanjani, maeneo ya kazi miongoni mwa sehemu nyingine.

1.8.1 Mbinu za ukusanyaji data

Katika utafiti wetu mbinu tulizotumia katika ukusanyaji data ni pamoja na kuusoma utenzi huu kwa ujumla na kuuelewa barabara. Kisha tulishughulika na kutambua dhana husika ambazo zipo chini ya vipengele hivi vya fani tunavyovishughulikia ambavyo ni matumizi ya tamathali za usemi pamoja na mbinu nyingine za matumizi ya lugha. Pia tumedurusu kazi kadha wa kadha maktabani ambazo tulizona zinaafikiana na uchambuzi wetu. Vile vile tumepitia tasnifu, vitabu, majarida na makala ya waandishi wengine yenye uhusiano na kazi yetu. Pia hatukudharau mwongozo tuliopewa na maulamaa wasimamizi wetu pamoja na wataalamu wengine ambao baadhi yao tuliwahoji. Pia tumepitia matini mbalimbali zilizoandikwa kuhusu nadharia tunayoitumia ya umuundo.

1.8.2 Uchanganuzi wa data

Baada ya kuusoma kwa makini utenzi tulioshughulikia, tulifanya tathmini yetu na tukachanganua data tuliyoikusanya. Uchanganuzi wetu umekuwa ni wa kielezi tu na si wa matumizi ya takwimu.

1.9 HITIMISHO

Katika sura hii tulianza na utangulizi ambapo tulieleza maana ya fasihi, matawi yake na tukaelezea mada tunayoishughulikia. Kwa kuwarejelea wataalamu mbalimbali wa fasihi tulitoa tafsiri mbalimbali za utenzi ukiwemo na mchango wetu. Kisha tulielezea tatizo la utafiti, madhumuni pamoja na nadharia tete tuljikita kwazo. Pia tulieleza sababu zilizotufanya sisi tuchague mada hii na tukaelezea upeo na mipaka ya kazi yetu. Tulizungumzia pia msingi wa kinadharia ya utafiti, yaliyoandikwa kuhusu somo hili, mbinu za utafiti ambapo mada yenyewe iligawika katika vijisehemu vitatu: Utangulizi, mbinu za ukusanyaji data na mbinu za kuchanganua data.

SURA YA PILI

2.0. UTANGULIZI

Kwa vile kazi yetu inahusu uchambuzi wa tamathali za usemi pamoja na mbinu nyingine za matumizi ya lugha ambapo ni miongoni mwa vipengele vya dhana pana ya fani, basi hatuna budi kuelezea fani ni nini, na pia kuvitolea maelezo baadhi ya vipengele vingine vya fani kikiwemo na kipengele hiki cha tamathali za usemi na mbinu nyengine za matumizi ya lugha.

2.1 DHANA YA FANI.

Mbatiah (2003:13) anasema; “ Dhana hii ina maana mbili. Kwanza, ni jumla ya vipengele vya kimuundo na kisanaa katika kazi ya kifasihi vinavyojenga kiunzi cha kujenga ujumbe na maana mahususi. Pili, ni kategoria ya fasihi, yaani utanzu kama ushairi, drama na riwaya.”

Vipengele vya kimuundo husaidia katika kuelezea mpangilio wa kazi ya kifasihi. Kwa mfano, katika kazi ya ushairi, unaweza ukaeleza muundo wa beti. Kwa mfano, shairi laweza kuwa ni la beti tatu, sita au kumi. Pia unaweza kueleza bahari ya shairi lenyewe na mengineyo. Kwa hivyo, tukimrejelea Mbatiah katika kuelezea maana ya kwanza ya dhana ya fani, itahusu umbo la kazi ya fasihi (hapa tunajikita katika bahari ya utenzi). Umbo la shairi ni muundo wa nje wa shairi na sifa za shairi huonekana kwenye umbo lake. Umbo la shairi hudhihirika machoni na hujumuisha beti, mishororo, mizani, vina moingoni mwa mengine.

Kwa mfano :

Bismillahi mbuyaza

awali ya kujifunza

sijui taufawaza

au vitanichachia (ubeti wa 1)

Umbo la shairi hilo ni bahari ya utenzi, na lina mishororo minne, vina vya ubeti huu ni *za, za, za*, na *ia*, lina mishororo minne katika ubeti na sifa nyinginezo. Maana hiyo ya pili itakuwa ni utanzu wowote ule wa kazi ya sanaa. Mbali na fasihi kuna na sanaa nyengine kama muziki, uchoraji, ufinyanzi, uchongaji vinyago na nyinginezo. Kwa hivyo, zote hizi nazo huitwa fani.

Wa Mutiso (2005:33) anasema kuwa, “fani ni jumla ya mbinu za kisanaa ambazo hutumiwa katika kuwasilisha ujumbe au maudhui katika fasihi.” Wamitila (2008:345) naye anasema, “fani ni jumla ya nyenzo zianazotumiwa kuwasilisha maudhui.” Naye Musokile (1993:57) anasema kuwa dhana ya fani ni vipengele vya kisanaa katika kazi ya fasihi. Anaendelea kusema kuwa ni vipengele vinavyojenga umbo la kazi ya sanaa. Mara nyingi vipengele vya fani ni pamoja na muundo, mtindo, mandhari, wahusika, na lugha. Pia anaongezea kwa kusema kuwa, si lazima vipengele hivyo vya kisanaa kujitokeza kwa uzito ule ule katika kila kazi ya kifasihi.

Maelezo haya yanatuelekeza kwenye dhana kuwa fani ni jinsi msanii anavyofinyanga umbo fulani ili kuelezea hisia zake kwa lugha ya ufasaha. Kwa mujibu wa maelezo ya wataalamu tuliowanukuu tunaona kuwa fani ni jumuisho la vipengele vyote vya fasihi

ambavyo msanii hutumia katika juhudi za kuelezea hisia au maoni yake kwa njia ya ufasaha.

Matokeo ya ujumuishwaji wa vipengele hivyo ni maudhui yanayowasilishwa kwa hadhira. Fani na maudhui hutegemeana na huathiriana kiasi kwamba bila ya fani maudhui yatakosekana na ili maudhui nayo yaweze kuwasilishwa ni lazima fani iwepo. Vipengele vinavyounda fani katika shairi ni vingi na baadhi yavyo ni lugha, muundo, wahusika, mtindo, mandhari, msamiati na vinginevyo.

Kwa maoni yetu kuhusu dhana hii ya fani ni; fani ni utumizi jumuishi wa mbinu za kisanaa katika kupitisha ujumbe kwa hadhira ikiwa ni kwa kupitia ushairi, tamthilia, riwaya au utanzu wowote wa fasihi.

2.2. LUGHA

Lugha ndicho chombo cha kubebea mawazo ya mtunzi kisanaa. Lugha vile vile ndiyo mali ghafi ya fasihi. Lugha inayotumika katika fasihi ikiwemo ushairi ni lugha ya kisanaa iliyopambwa kwa kusudi la kuibua hisia fulani kwa hadhira yake. Hisia zenyewe zinaweza kuwa ni pamoja na kuathiri nyoyo za hadhira kulingana na jinsi inavyotumiwa. Lengo la matumizi ya lugha yenyewe inaweza kuwa ni kuchekeka, kukejeli, kubeza kutia hamasa, kushawishi au kuchokoza. Kama Ndungo na Wafula (1993:50) walivyomnukuu Khatib (1981:16) kuwa lugha katika fasihi iwe andishi au simulizi, lazima iwe na utanashati na ulimbwende wa kipekee wenye mvuto na mnato wa kuteka na kuisimua hisia za wasikilizaji, wasomaji au watazamaji. Ili haya kutimia, inambidi mshairi kufanya uteuzi wa maneno na ayapangilie

kwa usanii mkubwa kwa madhumuni ya kujenga picha na tashbihi inayojenga maana na pia hisi kwa msomaji na msikilizaji.

Msokile (1993:86) naye anasema kuhusu lugha teule kuwa ni uteuzi wa maneno unaozingatia matumizi mazuri ya tamathali za usemi, rithimu, matumizi ya methali na kadhalika. Kipengele hiki cha lugha ni muhimu kwani ni baadhi ya vigezo vinavyotofautisha ushairi na tanzu nyinginezo. Katika ushairi, baadhi ya mambo ya kuangalia katika upande wa lugha ni pamoja na mpangilio wa maneno katika sentensi. Maswali ya kujiuliza hapa ni pamoja na: Kwa nini mpangilio huu wa maneno katika sentensi hii uko kama hivi ulivyo? Au, mpangilio wenyewe unatupa maana gani au hisia gani? Ama, je, mpangilio wenyewe unahusiana vipi na muundo wa shairi miongoni mwa maswali mengine.

Mfano:

Huna kazi ufanyayo, ela kuwatitimsha

Viumbe na **zao nyoyo, vitwa kuwagonganisha**

Hiino ndiyo kaziyo, yenye kukufurahisha

Ni kazi isokuchosha, **mno umeizoweya**

(Abdalla, A. 'Wasiwasi Enda Zako', *Sauti ya dhiki*, 1973:32)

Tukirejelea ubeti huo, mshororo wa pili na wa nne, tunapata kwamba kuna mpangilio wa maneno uliokiuka kaida za kisarufi. Mfano '**zao nyoyo**' badala ya '**nyoyo zao,**' '**vitwa Kuwagonganisha**' badala ya '**kuwagonganisha vitwa**', '**mno umeizoweya**' badala ya '**umeizoweya mno.**' Lau msanii angefuata kaida za kisarufi hangepata yale malengo yake ya urari wa vina na kazi yenyewe kwa yule anayeelewa ushairi ingekuwa

chapwaa. King'ei na Kemoli (2001:34) wanasema: "Ili kuweza kulielewa shairi barabara na kupata athari ya kila neno alilotumia mshairi, ni sharti msomaji wa shairi ajitahidi kupenya mawazo ya mshairi ili atambue sababu za mshairi kutumia maneno ayatumiayo."

Kwa hakika, ikiwa lengo la msomaji au msikilizaji wa ushairi litakuwa ni kupata ujumbe wa shairi lenyewe vile ilivyokusudiwa na mtunzi basi hana budi msomaji au msikilizaji huyo kulielewa shairi lenyewe barabara. Ukosefu wa uelevu huibua maana ambayo kamwe haikukusudiwa. Kwa hivyo, ikiwa maudhui ni kufunza, kuelekeza au kuonya. hayatakuwa yamemfikia mlengwa.

Kipengele kingine kinachoangaliwa katika lugha ni uteuzi wa maneno na semi. Maswali ya kujiuliza ni pamoja na ni kwa nini neno au usemi fulani umetumika katika shairi, au lau usemi huo utaondolewa katika shairi hilo patakuwa na athari gani?

Msokile (1983:56) akirejelea mashairi ya Saadani (1966:138) ametumia maneno teule katika shairi lake. Tazama mfano wa ubeti huu :

Nyoka amegutuka, ndani ya **shimo** kutuna

Tena amekasirika, hasira zenye kununa

Nyoka anababaika, **shimoni** kwa kujikuna

Siafu wamekazana, **nyoka** amekasirika

Tukirejelea ubeti huo wa shairi hili, msanii ametumia maneno *nyoka*, *shimo* na *siafu* kama wahusika. Hakika mhusika nyoka, siafu na shimo maana zao si zile za kawaida, bali hapa zimetumika kwa maana fiche. Kwa hivyo, kwa yule msomaji wa kawaida atapata maana tofauti, yaani hatapata ile maana halisi, lakini kwa yule

msomaji anayeimudu fasihi hususan ushairi, atapata ile maana lengwa. Chambilecho Sheikh Nabhany (1987) “Shairi hutumiwa kwa kufumba, kuichezea lugha kwa ujuzi na uhodari, kuhifadhia maneno mazito na magumu na vile vile katika mashindano na mapambano ya washairi.”

Lau mshairi hangepewa ule uhuru wa kutumia lugha katika ushairi basi ingekuwa ni kikwazo kikubwa sana katika utumiaji wa mbinu za uandishi na vipengele vingine vya fani.

2.3. UHURU WA KISHAIRI

Washairi wana uhuru wa kutumia lugha kinyume na matarajio ya kawaida. Ndio kusema ya kwamba mshairi anaamua kimakusudi kutofuata zile kanuni zinazoambatana na matumizi ya lugha.

Mbatiah (2001:95) anasema: “ Dhana hii ina maana mbili zinazohusiana. Kwanza, ni uhuru wa mshairi kukiuka kaida na kanuni za matumizi ya lugha katika viwango vya msamiati, sarufi, sintaksia, n.k. Pili, ni uhuru wa mwandishi wa utanzu wowote kukiuka sio tu kaida na kanuni za lugha bali pia kaida za kijamii na kweli za kihistoria.”

Tukijikita katika ule ufafanuzi wa kwanza, tunaona kuwa mshairi alistahiki kupewa uhuru huu, kwani kama angenyimwa basi ule usanii ungekosekana. Pia ingekuwa ni vigumu kwa msanii kupitisha maudhui yake kwa njia ya urahisi. Uhuru huu wa mshairi ni pamoja na kutumia maneno ya mkato, kurefusha maneno, kufupisha maneno, kubadilisha tahajia ya maneno na pia kutumia lahaja mbalimbali.

Kwa mfano :

Kuonake Mikidadi

mle katika **junudi**

mna **rijali wahidi**

Mikidadi **amuyua**

(*Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, ubeti wa 434)

Tukirejelea ubeti huo tunapata kwamba mshairi ametumia ule uhuru wake wa kishairi. Ametumia ufupisho katika kitenzi '**kuonake**' badala ya '**kuona kwake**'. Ametumia msamiati wa Kiarabu '**junudi**' badala ya '**jeshi**', '**rijali**' badala ya '**mwana mume**,' '**wahidi**' badala ya '**mmoja**.' Pia ametumia lahaja ya Kiamu '**amuyua**' badala ya lahaja ya Kiswahili sanifu '**amjua**.'

2.3.1. MSAMIATI KATIKA USHAIRI.

Msamiati ni maneno anayoyatumia msanii katika kazi yake. Msanii anaweza kutumia msamiati wa kilahaja, msamiati wa lugha ya kigeni kama vile Kiarabu, Kiingereza miongoni mwa lugha nyingine. Vilevile anaweza kutumia msamiati wa kale au hata wa lugha sanifu. Utumiaji wa msamiati pia hutegemea kile kipindi cha historia ambacho msanii anaandika kazi yake na pia maeneo ya Kijiografia ya msanii mwenyewe. Msanii akiwa amejumuika na jamii yenye mseto wa nasaba, basi hana budi kuathiriwa nazo kwa hivyo utumiaji wa msamiati wa lugha za nasaba hizo hana budi kuzitumia. Kwa vile mashairi ya kale kama vile *Utendi wa Herekali* na tendi nyinginezo kuna msamiati uliotumika katika tendi hizo ambazo kwa kipindi hiki hautambulikani, hatuwezi kusema ama mashairi hayo tuyapuuzilie

mbali kabisa au tuyashughulikie hayo peke yake. Ukweli ni kwamba katika mashairi ya kale kuna baadhi ya msamiati ambao hutumika hata katika mashairi haya ya kisasa.

Vile mshairi anavyouteua msamiati wake ni muhimu katika kuwasilisha ujumbe wake pamoja na athari za ujumbe huo kwa wasomaji au wasikilizaji wake. Msanii anaweza kutumia msamiati wa kawaida, anaweza kutumia msamiati wa maeneo fulani maalum au hata anaweza kutumia msamiati wa kale. Msomaji anahitajika kutambua kuwa maneno yanayopatikana katika shairi yamebeba ujumbe mzito na hata pengine kupata maana ya ziada.

Mshairi anapotumia maneno ya kale huwa ana sababu zake. Miongoni mwa sababu zenyewe ni pamoja na ulinganifu wa vina au mizani katika shairi, pia ni njia moja ya kuuhisha msamiati wenyewe, kukejeli hali au jambo fulani miongoni mwa sababu nyingine.

Mfano: Leo amka silale, silale leo amka
 Kushakucha kulichele, asubuhi ishafika
 Lete yako tuyaole, tujuwe yake hakika
 Nda kuliya nda kuteka?

(Abdalla, A. 'Jana na Leo na Kesho', *Sauti ya Dhiki*, 1973:42)

Katika ubeti huo, msanii ametumia msamiati wa zamani 'tuyaole', badala ya 'tuyaone' kwa lengo la kupata vina vya kati vilivyolingana. Mshairi pia anaweza kutumia maneno ya kawaida lakini yenye muundo usiokuwa wa kawaida. Kwa mfano, msanii anaweza kuyapa maneno sura nyingine kiumbo. Anaweza kuyafupisha kimaandishi au hata kuyarefusha. Mfano:

Kawapigia kelele

akiweta ndoni mbele

mume wangu **anitwale**

nami nipo **nangojea**

(Utendi wa Mikidadi na Mayasa, ubeti wa 18)

Tukirejelea ubeti huo mwandishi imembidi ageuze miundo ya maneno fulani kwa kusudi la kupata urari wa vina na mizani. Kwa mfano ametumia '**akiweta**' badala ya '**akiwaita**' '**anitwale**' badala ya '**anitwae**,' '**nami**' badala ya '**na mimi**,' '**nangojea**' badala ya '**ninangojea**.'

Katika kipengele hiki cha msamiati, msanii anaangaliwa kama ametumia msamiati wa kufumba ama msamiati ulio bayana. Aidha, kunaangaliwa kwa jinsi gani msamiati aliotumia msanii unafaa katika kutekeleza dhima ya kishairi. Uzito wa msamiati una umuhimu sana na cha kuzingatiwa hapa ni kama msamiati uliotumiwa umeweza kugusa hisia za hadhira au kama ni hafifu kiasi kwamba haukuweza kuamsha hisia za hadhira. Msamiati uliotokana na lahaja za Kingozi na ule uliotokana na lugha ya Kiarabu ndio uliosheheni katika mashairi haya ya Kiswahili ya zamani.

2.4 WAHUSIKA

Wahusika ni viumbe wanaotumiwa na msanii. Wahusika hutumiwa na msanii katika mtiririko wa matukio katika kueleza maudhui yake. Wahusika wanaweza kuwa binadamu, wanyama, wadudu, mizimu, misitu, shimo hata sauti. Wanatumiwa na msanii kusimamia hali mbalimbali za binadamu katika jamii wanamoishi.

Mbatiah (2001:109) anasema: “Wahusika ni watu tunaokutana nao katika kazi ya kifasihi na ambao kutokana na matendo na mazungumzo yao wanatudokezea kuhusu ujumbe wa kazi inayohusika.” Kutokana na ufafanuzi wa mtaalamu huyu, tungependa kuongezea kwamba, mbali na wahusika kuwa watu, pia kuna wahusika wanyama, wadudu, majitu, mashetani miongoni mwa wengine. Ujumbe anaotaja mtaalamu huyu si mwingine bali ni maudhui na maudhui hayo yanatekelezwa na vitushi vinavyojitokeza katika shairi kupitia kwa wahusika. Aidha wahusika ndio waneni, watendi na wawasilishaji wa mawazo ya mwandishi.

Msanii anaweza kumsawiri mhusika fulani akiwa na majukumu mepesi na kumsawiri mwingine akiwa na majukumu mazito. Hakuna kuzuka kwa mhusika kiajali tu bali kila mmoja wapo huwa ana jukumu la kutekeleza. Kwa mujibu wa King’ei na Kemoli (2001:54). “Ni nadra sana kutumia wahusika katika ushairi lakini zipo aina za tungo za kishairi zinazotumia wahusika hususan tenzi na mashairi ya masimulizi hasa mashairi ya kimapinduzi.” Nao Njogu na Chimera kwa mujibu wa Wamitila (2008:249) wanasisitiza hoja iliyotolewa na wataalamu wenzao King’ei na Kemoli, wanaposema kuwa, mashairi mengi hayana wahusika. Wanaendelea kusema kuwa, suala la uhusika au wahusika na mashairi linafungamanishwa kwa kiasi kikubwa na usimulizi. Tukijikita katika kauli hizi, hatutasema kwamba tumepotoka kwani hata hizi tenzi usuli wake ni masimulizi ukiwemo utenzi huu wa Mikidadi na Mayasa.

Wahusika hutumiwa kwa njia nyingi na kwa maumbile tofauti na wasanii. Maumbile hapa tunamaanisha viumbe vingine mbali na binadamu. Msanii anaweza

kumjenga mhusika kikamilifu na kusifu hali fulani. Vilevile anaweza kumtumia mhusika kubeza hali fulani. Msanii pia anatumia wahusika wadudu, wanyama na hata ndege kuchukua nafasi za wahusika halisi. Matendo wanayoyatenda wahusika hawa ni kama matendo ya binadamu halisi katika jamii. Msanii anapotumia wahusika wasiokuwa binadamu wa kawaida huwa ana lengo la kuwasilisha maudhui yake kimapumbo au huwa anachelea athari zitakazomkumba hususan akiwa katika mazingira yenye mfumo wa kisiasa asoiafikiana nao.

2.5 MANDHARI

Mandhari ni mahali au eneo ambapo jambo au tukio fulani linatendwa au kusimuliwa. Wamitila (2003:108) anasema: “Dhana hii hurejelea wakati na mahali pa hadithi au tamthilia, yaani mazingira ya utendaji wake na usimulizi wake.” Kwa hivyo, kutokana na maelezo ya mtaalamu huyu, tumepata aina mbili za mandhari. Mosi ni mandhari ya mahali mfano mjini, shambani, afisini, na penginepo. Mandhari ya aina ya pili ni ya wakati yaani mandhari ya wakati fulani kihistoria. Kwa mfano, tukijikita katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa* tunapata kwamba matukio ya utenzi huu yalitokea katika enzi za tawala za kifalme zilipokuwa zimeshamiri, wakati ambapo mambo ya utabaka yalikuwapo. Enzi ambazo koo fulani zilikuwa zikienziwa sana katika jamii huku nyingine zikidunishwa.

Katika kusoma kazi ya fasihi, msomaji huweza kuwazia kazi yenyewe ni ya kipindi fulani katika historia kwa kurejelea vifaa vinavyotumika katika kazi yenyewe.

Kwa mfano, matumizi ya panga na farasi katika utendi huu hutudhihirishia kuwa ni wa kipindi cha kale. Pia hutudhihirishia kuwa matukio yenyewe yalitokea sehemu za Uarabuni. Katika kipindi hiki kulikuweco waungwana na watumwa, pia dini ya Kiislamu ilikuwa haijashamiri sawa sawa. Tazama mifano :

Kenda mpangia nyumba
njema iliyokupambwa
wasichana na wachumba
na waungwana jamia

Na jamii wavulana
ambao ni waungwana
muyini wakakutana
Mikidadi kumwendea

(Utendi wa Mikidadi na Mayasa, ubeti wa 658 na 659)

Kutokana na beti mbili hizo, tumeweza kung'amua kuwa mazingira yanayodhihirika ni yale ya kitabaka. Kuna watu wa tabaka la juu na la chini, waungwana na watumwa. Aidha mandhari ya kijiografia pia yamesheheni katika utenzi huu. Kazi nyingi za fasihi zina mandhari yanayobainika wazi ukiwemo ushairi.

2.6 TONI

Toni ya shairi ni jinsi sauti ya msomaji shairi inavyosikika na msikilizaji. Yaani ni ile namna msomaji wa shairi anavyosema jambo fulani. Msomaji anaweza kusoma kwa furaha, au kwa huzuni. Toni hufungamana kwa kiasi kikubwa na maudhui

anayozungumzia mshairi. Kama ujumbe katika shairi ni kuhusu dhuluma basi toni ya shairi lenyewe itakuwa ni ya uchungu. Tazama mfano huu:

Kijana kakiadhibu
kwa pingu na makulabu
kafanya yake sababu
mkewe kumtwalia

(*Utendi wa Mikidadi na Mayasa*, ubeti wa 191)

Katika ubeti huo toni iliyotumika ni ya uchungu. Tazama mfano mwengine:

Onani mato onani mumtizame Muyaka
Yuenda msikitini kipindi kisijatoka
Yuaja ngia nyumbani Ijumaa akishuka
Muda jua kipinduka t'aoneka mandamoni.

(Abdulaziz M.H. 'Harusi ya Bwana Muyaka', *Muyaka*, uk. 278, ubeti wa 4)

Toni iliyotumika katika ubeti huu ni ya furaha. Mfano mwengine wa toni ya uchungu ni:

Wanatumkanyaga binadamu, bila ya kuhisi
Hutuponda na kutuhujumu, bila ya kisisi
Maisha yetu ni madhulumu, kupotea basi
Sababu sisi ni sisimizi.

(Mohamed, S.A. 'Sisimizi Sisi', 'sikate tamaa (1980:19)

2.7 MUUNDO

Muundo ni jumla ya viungo vinavyowekwa pamoja na kuunda kitu na kuwa kamili. Katika ushairi, muundo ni vile vipengele vya fani vinayowekwa pamoja na kuunda muundo. Wamitila (2003:215) anaeleza kuwa muundo ni neno pana ambalo hujumuisha

mjengo wa shairi, yaani jinsi linavyoonekana. Maelezo haya yanaelekea kuwiana na maelezo yetu. Upana wa shairi hapa unamaanisha kuwa ili shairi kupata utimilifu wake ni mpaka kupatikane vijenzi vingine vingi, viletwe pamoja na upatikane huo muundo. Kama ilivyo katika sanaa kama ya uashi, fundi huhitaji vifaa mbali mbali vichanganywe pamoja na kusimamisha jengo.

Shairi huwa na muundo wa aina mbili, wa ndani na wa nje. Muundo wa nje ambao pia huitwa umbo, huwa unadhihirika machoni kwa maana huwa unaonekana na hujumuisha dhana kama vile beti, mizani, mishororo, vina, kibwagizo na vinginevyo. Mfano katika utenzi wa Mikidadi na Mayasa:

Bismillahi mbuyaza

awali ya kujifunza

sijui taufawaza

au vitanichachia (ubeti wa1)

Maelezo tutakayotoa kuhusu maandiko hayo ni kwamba huo ni ubeti wa utenzi, una mistari minne, una mizani katika kila mstari, una vina *za, za, za*, na *ia* na mengineyo. Muundo wa ndani wa shairi nao unadhihirika akilini mwa msomaji au msikilizaji. Muundo huu nao hujumuisha dhana kama mtiririko wa maneno, mpangilio wa shairi, maudhui, lengo, mafunzo na mengineyo.

2.8 MTINDO

Mtindo ni zile mbinu za kipekee zinazotumiwa na mshairi katika kutunga shairi lake. Dhana hii ya mtindo inarejelea zile sifa za kipekee alizonazo mwandishi wa fasihi kwenye kazi yake. Mtindo humtambulisha mtu. Tunachomaanisha hapa ni kwamba,

hadhira huenda ikazowea ile mitindo anayotumia mwandishi fulani kiasi kwamba unaposoma kazi fulani mara moja ukaweza kuishabihisha kazi hiyo na mtu fulani bila hata ya kutajiwa jina lake.

Mtindo katika shairi huhusisha: Mishororo, upangaji wa semi, maneno na mawazo, kupindua kaida za maneno, kama vile; *aliye juu mngoje juu*, miongoni mwa mengine. Kwa ufupi mtindo unajumuisha muundo na ndipo hapo ushairi huchanaganuliwa kwa kutumia vigezo hivyo tulivyoviorodhesha hapo juu na vinginevyo. Aidha msanii anaweza kutumia mseto wa mitindo. Tutataja tu japo kwa mukhtasari sifa ambazo mtunzi wa *Utendi wa Mikidadi na Mayasa* kwa kurejelea baadhi ya beti au mishororo ya utenzi huu. Mifano ni pamoja na:

Mtindo wa kuzigawa beti au mafungu ya beti kadhaa zikawa zinazungumzia mada kadhaa, kwa mfano ubeti wa 1 anaanza kwa kumtaja Mungu. Katika ubeti wa 2 - 4 anaelezea ule udhaifu wa kibinadamu alionao na kwamba lau tutaona makosa tusimtie aibu. Tazama mifano hiyo:

Kwa kuwa sina makini
sina fahamu moyoni
kwa dunia kuwa duni
tangu sasa nawambia (ubeti wa 2)

nawambia tangu sasa
mambo kabisa kabisa
msije ona makosa
aibu mkanitia (ubeti wa 3)

Mkanitia aibu

pasi kuwa na sababu

kunitoa ni thawabu

nami hazidi kwelewa (ubeti a 4)

Dibaji hiyo yaendelea hadi kuishilia ubeti wa 11 na ubeti wa 12-60 ndio tunaelezwa kuhusu uposi wa Mayasa na mengine mengi yanaendelezwa katika mafungu mengine ya beti. Mtunzi pia amefuata mtindo wa kusawiri matabaka katika jamii (ubeti 659). Tazama mfano:

Na jamii wavulana

ambao ni waungwana

muyini wakakutana

Mikidadi kumwendea (ubeti wa 659)

Jamii hii iliyozungumziwa ni ya Kiarabu na mfumo huu ulikuwako na hata upo katika baadhi ya nchi za Kiarabu. Washairi waliokuwako katika nyakati hizo walikuwa wakiwasifu na kuwaenzi sana mashujaa na viongozi huku lile tabaka la watumwa likidhulumiwa.

2.9 TAMATHALI ZA USEMI

Tamathali za usemi ni ukiushi wa kimakusudi wa matumizi ya lugha hasa katika kiwango cha kisemantiki na kisintaksia, ili kuleta msisitizo au maana mpya. Matumizi ya tamathali za usemi humwezesha mshairi kusema au kuandika anachotaka kuandika na kumwathiri msikilizaji au hadhira. Mbali na hili, tamathali za usemi humwezesha mshairi kupitisha maudhui yake yaliyo makali, mazito na nyeti bila ya kuleta hujuma yoyote. Aidha matumizi ya tamathali za usemi huzusha

tanabuhi kwa hadhira na mihemko yao na kuwapatia uwezo wa kutafakari na kutekeleza wanachopaswa kutekeleza. Katika utenzi huu wa Mikidadi na Mayasa, mtunzi ametumia ainati za tamathali za usemi. Baadhi yazo zinafanana na kuingiliana na nyengine kutofautiana. Vile vile msanii huyu ametumia tamathali za usemi zaidi ya moja katika ubeti mmoja. Haya yanadhihirika katika beti kadhaa. Pia kuna matumizi ya tamathali za usemi au mbinu nyingine za matumizi ya lugha ya aina hiyo moja tu ambayo imetumika katika kila mstari mmoja wa ubeti husika,

mfano: Enendani enendani
 upesini upesini
 mpateni mpateni
 asubuhi tauawa (ubeti wa 722)

Katika ubeti huo, msanii ametumia takriri neno ambapo katika mstari wa kwanza wa ubeti amerudia kitenzi ‘enendani’ mara mbili, mstari wa pili amerudia kielezi ‘upesini’ na mstari wa tatu, ametumia kitenzi ‘mpateni’

Wengi wa wataalamu wametumia na kutoa fafanuzi tofauti tofauti za tamathali za usemi kwa malengo ya kufaa mahitaji yao. Kwa maoni yetu, twaona ipo haja ya kuweka bayana mambo haya. Tamathali za usemi zilizotumiwa hapa ni nyingi mno ijapokuwa kuna baadhi ambazo hakuna kama vile **methali**. Kwa hivyo, tutazitolea maelezo zile tu ambazo tumezipata hapa.

2.9.1 TASHBIHI

Tashbihi pia huitwa tashbiha. Huu ni ulinganishi wa moja kwa moja. Katika ulinganishi huu, kitu kimoja, vitu au hali mbili na hata zaidi hulinganishwa na kitu kimoja kwa

kutumia viuganishi kama, ja, mithili ya, mfano wa, fanana na, kama, sawa sawa na, kuliagana na, na vinginevyo. Kufanana huku huwa ni kwa ushabihiano wa hali ya utendaji au maumbile kama vile kimo, udogo, unene, sura na mengineyo. Kwa mfano mtu akiwa amekonda utamfananisha na ng'onda kwa maana mwili wake hauna nyama umekauka au hata unamfananisha na sindano kwa maana ni mwembamba sana, ndipo pale tunasema “amekonda kama ng'onda.” Au “mwembamba kama sindano.” Dhamira moja ya ulinganishi huu ni kuisisitiza sifa fulani na pia kutujengea picha ya aina fulani akilini.

2.9.1.1 SITIARI

Hii ni tamathali ya usemi ambayo inahusu ulinganishi usiokuwa wa moja kwa moja. Katika tamathali hii, kitu, matendo ya kitu au vitu vyenye tabia iliyofanana hulinganishwa. Tofauti na tashbiha, sitiari haitambulishwi kwa kutumia viungo kama vile kama, ja, mithili ya na vinginevyo bali sifa ya kitu fulani huelezwa kwa kusema kwamba kitu hicho ni kingine. Mfano, ‘David Rudisha ni simba.’

2.9.1.2 MASWALI YA BALAGHA

Balagha ni tamathali inayohusu kuuliza maswali ambayo hayahitaji majibu, kwa sababu majibu yenyewe huwa yako wazi kwa kila mtu. Mtunzi hutumia maswala haya ili kuisisitiza ujumbe anaotaka kuupitisha. Nia ya mtunzi katika maswala kama haya huwa ni kufafanua zaidi wazo au mawazo husika na vile vile kutoa msimamo wake pamoja na kumshawishi msomaji na msikilizaji. Maswali kama haya huamsha nadhari ya msomaji na kumfanya atafakari zaidi juu ya

kinachozungumziwa. Mtunzi huyatumia maswali haya ili kuwachochea wasomaji na wasikilizaji wake waweze kufikiria zaidi juu ya jambo analolieleza.

2.9.1.3 KEJELI

Katika tamathali hii ya kejeli au kijembe mtunzi au msemaji hutumia ili kumtweza au kumdunisha mtu au hali fulani. Maneno yanayotumiwa huwa ni ya kukata, ya kuchoma na ya kutia uchungu. Mtu anapobandikwa sifa ambazo hastahili kuwa nazo, huwa anakejeliwa. Maneno yanayotumiwa katika tamathali hii kwa kawaida huwa ni kinyume kabisa na maana inayotakiwa kutoa maneno hayo. Katika ushairi msanii anapokejeli, hutarajia msomaji ndiye mwenye kupekua na kuelewa maana fiche iliyofichwa aliyokusudia kuwasilisha.

2.9.1.4 CHUKU

Katika tamathali hii, jambo fulani hukuzwa kupita kiasi au kudunishwa sifa hizo kuliko hali yake ya kawaida. Kukuzwa huko kunaweza kuwa kwa ukubwa au kwa udogo, kwa wingi au kwa uchache. Kwa msingi huu basi huwa pana ukinzani kati ya hali inayosemwa na ukweli wenyewe. Kupiga chuku ni kutia chumvi. Tamathali hii hasa husisitiza ujumbe unaowasilishwa na wala haitumiwi kwa nia mbaya. Katika kazi ya fasihi tamathali hii inapotumiwa huleta athari za kimguso kwa msomaji na msikilizaji na hupusha uchovu wa akili inaposababisha kicheko

2.9.1.5 TASHIHISI

Katika tamathali hii kitu kisichokuwa na uhai hupewa uhai na sifa za kibinadamu. Tamathali hii pia huitwa uhuishaji ama uhuishi

2.9.1.6 DHIHAKA

Katika tamathali hii, hisia za mtunzi kumuhusu mtu au kuhusu kitu au hali fulani hufichwa. Kimsingi huwa pana kinaya katika maneno yaliyotumiwa. Sababu kuu ya dhihaka ni kuchekesha na kukera au kumbeza mtu au hali.

2.9.1.7 LAKABU

Asili ya neno hili ni lugha ya Kiarabu, 'lakab'. Lakabu ni sifa anayopewa mtu au ajipaye mtu yeye mwenyewe kwa sababu ya tabia fulani ya kipekee. Aidha ni jina la kubandikwa, ambalo muhusika hupewa au kujipa mwenyewe. Katika ulimwengu wa kishairi kuna watunzi kadha ambao aidha wamejipa au kupewa lakabu. Kwa mfano, Mshairi Mwalimu Hassan Mbega anajulikana kwa lakabu ya 'Ustadh Shuara'

2.9.1.8 MAJAZI

Katika mbinu hii mtunzi humpa muhusika wa fasihi, mahali, kitu au jambo jina linalofanana na tabia au sifa yake. Majina ya kimajazi husimamia maana maalum.

2.9.2 MBINU NYINGINE ZA MATUMIZI YA LUGHA

Mbali na tamathali za usemi, mwandishi pia ametumia mbinu nyingine za matumizi ya lugha ambazo ni muhimu pia. Mbinu zenyewe ni pamoja na, takriri, tabdila, visawe, usambamba miongoni mwa nyengine.

2.9.2.1 TABDILA

Tabdila ni ukiushi wa kifonetiki. Katika mbinu hii, mtunzi hubadilisha sauti fulani katika neno kwa lengo la kuleta uwiano fulani, hususan katika kipande cha mwisho

cha mshororo. Hili hutokea kwa lengo la kupata kina kifaacho. Katika mbinu hii maneno huendelezwa kwa njia tofauti na vile ilivyozoeleka. Mfano:

Waliokuja waposi
kumuonakwe Mayasi
yumo juu ya farasi
Jabiri wakamwendea (ubeti wa 27)

Katika ubeti huo mshororo wa pili, neno ‘Mayasi’ limetumika badala ya ‘Mayasa.’ Lau angetumia Mayasa, hakungekuwako ule urari wa vina.

2.9.2.2 INKISARI

Katika mbinu hii, maneno hufupishwa kwa kudondosha silabi katika neno kwa lengo la kupata kina maalum au kutosheleza mizani. Ukiushi huu ni wa kimofolojia. Mfano:

Nawambia tangu sasa
mambo kabisa kabisa
msije ona makosa
tangu sasa nawambia (ubeti wa 3)

Katika mstari wa kwanza, wa tatu, na wanne wa ubeti huu inkisari imetumika katika maneno yafuatayo na kusababisha tofauti hii: ‘Nawambia’ badala ya ‘ninawaambia,’ ‘msije ona’ badala ya ‘musije mukaona’ na ‘nawambia’ badala ya ‘ninawaambia.’ Kwa hivyo katika neno ‘ninawaambia’ silabi ‘ni’ imedondoshwa na neno lenyewe kuwa ‘nawambia,’ katika maneno ‘musije mukaona’ silabi ‘u’ imedondoshwa katika ‘musije’ na silabi ‘mu’ na ‘ka’ zimedondoshwa katika ‘mukaona’ na kubaki ‘ona’ na mwisho silabi ‘ni’ imedondoshwa katika neno ‘ninawaambia’ na kuwa ‘nawambia’

2.9.2.3 MAZIDA

Katika mbinu hii, mtunzi aghalabu hurefusha maneno kupitia kuongeza silabi kwa lengo la kutosheleza idadi ya mizani katika mshororo au kufikia kina fulani kinachohitajika. Ukiushi huu nao pia ni wa kimofolojia. Mfano:

Waliokuja waposi

kumuonakwe Mayasi

yumo juu ya farasi

Jabiri wakamwendea (ubeti wa 27)

Neno 'kumuonakwe' limerefushwa. Lau neno hili halingerefushwa, nakuandikwa kama inavyotakikana 'kumuona' basi mizani za mshororo huu hazingekuwa sawa na za mshororo ile mengine ya ubeti huo. Mshororo huo ungekuwa na mizani saba badala ya nane.

2.9.2.4 TAKRIRI

Katika mbinu hii ya lugha, mshairi husisitiza au hushadidia kimakusudi ujumbe unaohusika, ili msomaji apate athari ya msisitizo, kama vile mdundo katika ushairi. Mshairi hutumia irabu, konsonanti, silabi, neno, mshororo na hata maana fulani kwa minajili ya kusisitiza jambo. Kwa maana hii, kuna aina kadha za takriri kama vile takriri irabu, takriri konsonanti, takriri silabi, takriri neno, takriri kibwagizo na hata takriri mshororo.

2.9.2.5 UKIUSHI WA KISARUFI

Hii ni ile mbinu ya kukiuka mpangilio sawa wa maneno katika sentensi kwa lengo la kusawazisha vina. Hapa unapata mtunzi anageuza ule mpangilio wa kawaida wa maneno katika mishororo ya shairi kimakusudi kwa nia ya kutimiza urari wa vina.

Mfano:

Nawambia tangu sasa
mambo kabisa kabisa
msije ona makosa
aibu mkanitia (ubeti wa 3)

Katika ubeti wa 3 hapo juu, mshororo wa 4, msanii alikiuka sarufi kwa kuendeleza ‘aibu mkanitia’ badala ya ‘mukanitia aibu.’ Kama angetumia ‘mukanitia aibu,’ vina havingelingana.

2.9.2.6 TASWIRA

Taswira ni picha ya mahali au kitu fulani inayojichora mawazoni mwa msomaji au hata msikilizaji, kutokana na maelezo anayopata katika kazi ya fasihi. Picha hii huwa kama picha halisi kwa msomaji au msikilizaji. Kupitia kwayo msomaji huhisi, hugusa, huonja, na kuona yanayoelezwa. Taswira huweza kuundwa kwa njia si haba za kisanaa kama vile semi, maelezo, ishara, tashbihi miongoni mwa nyingine. Ujenzi au uundwaji wa taswira humfanya msomaji au msikilizaji apate aina mbalimbali za hisi zinazoshughulikiwa na kazi ihusikayo ya kifasihi; yaani hisi za kunusa, kuona, kugusa, kuonja na kusikia .

2.9.2.7 MISEMO

Misemo ni kauli za mafumbo. Kauli hizi zimeundwa kwa kutumia maneno ya kawaida yaliyositiri maaana ya ndani. Misemo huambatana na utamaduni husika. Huku ni kusema kwamba kila utamaduni umefungamana na misemo inayowahusu, iliyoafikiana na itikadi, mila na desturi na mazingira yake. Kwa hivyo matumizi ya misemo katika fasihi hutegemea uhai wake katika matumizi yake katika jamii, tukitilia maanani kwamba misemo aghalabu huweza kufa kama ilivyo misimu. Kwa vile misemo huambatana na jamii, hivyo basi jamii husika huielewa kwa undani na kwa uzito unaostahiki kwani hubeba mafunzo kwa jamii husika.

2.9.2.8 USAMBAMBA

Usambamba ni mbinu ya urudiaji wa muundo sawa wa kisintaksia katika virai, kishazi, au sentensi. Katika mbinu hii mtunzi anaweza kutumia maneno au hata semi mbili zinazokinzana kimaana kwa lengo la kusisitiza ujumbe. Kuna usambamba wa kimaana, kidhamira, kisintaksia, na aina nyinginezo.

2.9.2.9 VISAWA

Visawe hutumiwa kufanya kazi ya kutilia mkazo wazo, dhana, au maana fulani ya ujumla kwa kuibainishia maneno yenye maana ndogondogo za karibu. Visawe ni maneno ambayo yako katika kikoja kimoja cha maana. Katika ushairi, hii ni mbinu muhimu kwa sababu hupunguza ule uchovu wa matumizi ya maneno yayo kwa hayo kila wakati..

2.9.2.10 MBINU REJESHI

Mbinu hii pia huitwa kisengere nyuma. Katika mbinu hii, mtunzi huyaeleza matukio yaliyotokea hapo awali. Ni mtunzi mwenyewe huwa ndiye anayehadithia habari yenyewe ama muhusika anayechaguliwa na mtunzi. Mbinu hii huziba pengo lililoachwa kuhusu habari ya muhusika, au matukio yasiyo dhahiri au hata hali za wahusika.

2.9.2.11 UTOHOZI

Katika mbinu hii mtunzi huchukua neno la lugha fulani na kulipa neno hilo mwendelezo wa lugha pokezi. Lengo la mtunzi kutumia mbinu hii ni kwamba huwa hataki kupoteza maana ya ujumbe uliodhamiriwa au kukosa neno la kutumia katika lugha anayoitumia.

2.9.2.12 TAHARUKI

Hii ni ile hamu na matarajio msomaji anayokuwa nayo kutaka kujua kitakachotokea au kufuatia katika kazi anayoisoma. Athari ya mbinu hii ni kumtia msomaji mshawasha ili atake kuendelea kusoma zaidi.

2.9.2.13 NAHAU

Nahau hutumiwa kuelezea kauli zilizoundwa kwa lugha ya kawaida lakini iliyoficha maana au maaana yenyewe isiyokuwa ya kawaida. Aghalabu nahau hujumuisha kitenzi na jina. Nahau ni kikolezo kuitia utamu lugha inayohusika.

2.9.2.14 HITIMISHO.

Katika sura hii tumefafanua fani pamoja na kuvitaja baadhi ya vijenzi vya fani katika kazi ya fasihi haswa tenzi na pia kuvitolea maelezo kwa kina. Tumewanukuu baadhi ya wanavyuoni kwa kuhusisha maoni yao kuhusu vijenzi hivyo vya fani na vile vile tumetoa maoni yetu kuvihusu. Mbali na hayo tumeweza kuzitaja tamathali za usemi pamoja na mbinu nyingineza matumizi ya lugha tulizoweza kuzipata katika utenzi huu wetu tunaoshughulikia na pia kuzitolea maelezo. Tuna wingi wa matumaini kwamba maoni yao na yetu yametoa msingi mwema katika kuufahamu utenzi tunaoushughulikia.

SURA YA TATU

3.0 TAMATHALI ZA USEMI

Tamathali za usemi ni ukiushi wa kimakusudi wa matumizi ya lugha hasa katika kiwango cha kisemantiki na kisintaksia, ili kuleta msisitizo au maana mpya. Matumizi ya tamathali za usemi humwezesha mshairi kusema au kuandika anachotaka kuandika na kumwathiri msomaji au msikilizaji. Katika utendi huu kuna tamathali za usemi kadha ambazo zimetumika.

3.1.0 TASHBIHI

Msanii ametumia tashbihi ili kufafanua zaidi anachokizungumzia. Tashbihi humsaidia msomaji kufahamu vizuri vile vitu au hata hali zilizolinganishwa kwa vile tokeo lake ni uchoraji wa picha fulani akilini mwa msomaji ama msikilizaji. Mwandishi amezifananisha sifa za mtume Muhammad na maji ya bahari jinsi zilivyo nyingi. Maji ya bahari yamechukua sehemu kubwa kimaeneo... **kama mai ya bahari...**(mfano wa maji ya bahari – ubeti wa 10). Mwandishi anausifu uzuri alionao Mayasa na anayafananisha macho yake yalivyong'ara na macho yaliyopakwa wanja. Macho yaliyopakwa wanja huvutia...**kama wanda wa kutiwa...**(mfano wa wanja wa kupakwa machoni- ubeti wa 18). Wanda ni lahaja ya kiamu. Pua ya Mayasa vile ilivyosimama na kunyooka inafananishwa na upanga wa chuma na anaposema kinywani mwake mnanukia manukato. ...**kama upanga wa chuma...**(mfano wa upanga wa chuma- ubeti wa 20. Mikidadi anaelezea kuwa jinsi Mayasa anavyopigana ni sawa na vita vitakatifu vya jihadi... **niwene kama jihadi...**(nimeona kama vita vya kutetea

dini – ubeti wa 67). ‘Niwene’ ni lahaja ya Kitikuu na neno lenyewe lina maana ‘nimeona’. Tashbihi nyingine ni kama zifuatazo: ... **kama simba alokaa...** (mfano wa simba aliyekaa – ubeti wa 282). Mikidadi anaitwa mtoto muasi na kufananishwa na simba aliyekaa. ...**mkali kama asadi...**(mkali mafano wa simba –ubeti wa 301). Jinsi vile Mikidadi alivyo mkali anafananishwa na simba. Simba ni mnyama mkali na shujaa na katika hekaya nyingi anaitwa mfalme. Mikidadi naye ni shujaa. Asadi ni neno la Kiarabu lenye maana ya simba. ...**kama kidole na pete...**(mfano wa kidole na pete – ubeti wa 320). Mshairi anaeleza jinsi Mikidadi alivyokuwa amezingirwa na wale Wamanga na kukaribiana sana mfano wa kidole na pete vilivyokaribiana... **kama wingu la mvua...** (mfano wa wingu la mvua – ubeti wa 583) Mwandishi anafananisha vile vumbi na upepo ulivyotanda kila mahali, vumbi amabalo lilisababishwa na vita...**wakele kama jabali...**(wamekaa kama jabali bila ya kuzunguka huku wala kule, yaani tuli – ubeti wa 584)...**kama kula matikiti...**(mfano wa kula matikiti- ubeti wa 756). Yaani kina Mikidadi waliweza kulikabili jeshi kwa urahisi sana. ... **ni kama kuku na mwewe ...** (ni mfano wa kuku na mwewe – ubeti wa 757) Mwandishi anamaanisha walikuwa mbali mbali kila mtu upande wake. Kwani pindi kuku amuonapo mwewe mara nyingi hujitenga ili akimbie hujuma ya kutoka kwake yeye na vifaranga wake.

3.1.1 SITIARI

Hii ni tamathali inayohusu ulinganishi usiokuwa wa moja kwa moja. Katika sitiari, kitu Fulani husemwa ni kingine. Katika utenzi huu, sitiari kadha zimetumiwa kuwalinganisha baadhi ya wahusika. Mwandishi amewalinganisha Mikidadi, Hamza, Abasi na Sayyidina Ali na vitu au viumbe mbalimbali. Katika baadhi ya beti mwandishi amewapa nafasi

wahusika wajilinganishe wao wenyewe na vitu au viumbe. Aidha mwandishi pia amewapatia nafasi wahusika wengine wawalinganishe wahusika wenzao na viumbe wengine. Kwa mfano, yule mfalme baada ya askari wake kupigwa na Mikidadi anawalinganisha na zikuku yaani vifaranga. ‘Zikuku’ ni lahaja ya Kiamu. Katika lahaja hii, aghalabu maneno yanayoanza na sauti ‘v’ katika Kiswahili sanifu, sauti hiyo hudondoshwa na nafasi yake kuchukuliwa na sauti ‘z’. Kwa hivyo mfano neno vitu litakuwa zitu kama vile neno vikuku likawa zikuku. Sitiari hizi huwasaidia wasomaji kukisia uwezo na ujuzi walionao wahusika hawa. Baadhi ya sitiari zilizotumika ni:...

Simba amewangilia...(Shujaa amewaingilia, Mikidadi amejilinganisha na simba, yaani shujaa – ubeti wa 208)...

ndimi simba ndimi tui...(Mikidadi anajilinganisha na simba na chui – ubeti wa 221). ‘Tui’ ni lahaja ya Kiamu kumaanisha chui. Sifa za wanyama hawa zinasimamia ushujaa. ...

Simba wa Mola twaa...(Hamza ami yake Mtume Muhammad S.A.W analinganishwa na simba aliye mtiifu pia –ubeti wa 253)...

naye ni simba mtesi...(Abasi ami yake Mtume Muhammad(S.A.W.) analinganishwa na simba mtesi, yaani simba anayependa vita- ubeti wa 255) ..

ndimi farasi adui...(Ni mimi farasi adui, Mikidadi anajilinganisha na farasi adui-ubeti wa 294). Farasi adui anaweza kukupiga mateke, akakuuma, akakukanyaga na kukuangamiza....

ni mimi simba wa mwitu...(Mikidadi anajilinganisha na simba wa mwitu – ubeti wa 295) Mikidadi alipokuwa katika zile harakati zake za kusaka mahari ya Mayasa alijiamulia kukaa barani msituni. ...

ewe shujaa asadi...(Amiri anamlinganisha Mikidadi na simba aliye shujaa – ubeti wa 338)...

kaweta enyi zikuku...(kawaita e nyinyi vifaranga. Mfalme aliwalinganisha askari wake na vifaranga vya kuku pale walipopigwa na Mikidadi – ubeti wa 402)...

ndimi simba wa Muungu...(Sayyidina Ali,

mkwe wake Mtume Muhammad S.A.W. anajilinganisha na simba wa Mungu – ubeti wa 599). Sifa hii ya kuitwa simba wa Mungu inadhihirika katika kila hutuba au darasa za kiislamu pale Sayyidina Ali anapotajwa anatajwa kwa lakabu ya simba wa Mungu. ...ewe simba mnafisi... (ewe simba mwenye nguvu. Mayasa anamlinganisha Sayyidina Ali na simba mwenye nguvu – ubeti wa 620).

3.1.2 MASWALI YA BALAGHA

Maswali haya huulizwa na mwandishi ili kuisitiza ujumbe anaoupitisha kwa hadhira. Yanaulizwa kwa minajili ya kuitanabahisha hadhira, kuichochea na ili iweze kufikiria zaidi juu ya maudhui anayoyapitisha. Maswala haya huwa hayahitaji jibu. Yafuatayo ni baadhi ya maswali ya balagha yaliyotumiwa katika utenzi huu.

Hughani akiomboa
ni yupi mtaka ndoa
anitakae kuo
napenda kumwangalia (ubeti wa 26)

Husema akijighani
alijuu farasini
wawapi mashujaani
watamano kuo (ubeti wa 34)

Maswali hayo mawili yanaulizwa na Mayasa na yanawalenga wale waposi wake. Maswali yenyewe yanachokoza hisia na kuzua changamoto kali kwa waposi ambao yeye Mayasa anajua wazi kuwa wapo ila pengine ni idadi yao tu ndio asiyojua. Na yumkini anataka kusema kwamba yeye ndiye shujaa. Cha msingi hapa ni kwamba Mayasa hataki

mume mwenye mali, bali anataka mume atakaye mshinda kivita. Kwa hivyo licha ya yeye kujua kuwa watu hao wapo, na kwamba kuna na wale waliobarikiwa mali lakini mali peke yake haikutosha kumpata yeye. Watu waliokuja kwenye nikaha walishangazwa sana na Mikidadi jinsi alivyokuwa jasiri na kuweza kupigana na watu wengi vile. Walimfananisha na luhani, mwana wa jini, sheitani na hata malaika. Nikupitia ushujaa wake ndipo maswala haya mengi yakaulizwa. Mfano:

kamuuza sultani

ewe waziri unani

unasubiwa na jinni

na maradhi kukungia (ubeti wa 465)

Katika ubeti wa 465 Sultani anamuuliza waziri wake lile alilo nalo, ama mefikwa na nini. Anamuuliza kama amefikwa na jini ama amefikwa na maradhi. Ukweli ni kwamba Sultani anajua kile kilichomkasirisha waziri wake. Ni lile tendo la kuvuliwa taji. Katika ubeti wa 509, Jabiri anarudia kwa kumuuliza Turadi kuhusu pale Mikidadi alipo na kwamba siku alizotoa za kutafuta mahari zimeshatimia. Ukweli ni kwamba Turadi anajua kuwa Mikidadi anashughulika na kukusanya mahari ili amuo Mayasa na kuchelewa kwake ni pengine hajaafanikiwa.

3.1.3 KEJELI

Tamathali hii hutumiwa katika kumtweza au kumdunisha mtu au hali fulani. Maneno yanayotumiwa huwa ni ya kutia uchungu, ya kutamausha na ya kukata. Katika utenzi huu Mikidadi amekejeliwa na kusemekana kwamba hana kitu, akili yake haikutua, mtu wa pepopepo, hana akili na hata akipewa muda wa kuchuma mahari hatatimiza na

mengine mengi. Kejeli zote hizi alizofanyiwa Mikidadi kamwe hazikufua dafu kwani mwishowe aliweza kukusanya mahari aliyoahidi. Katika baadhi ya beti ambazo kejeli imetumika ni pamoja na:... **huyu ni mwana yatima...**(Mikidadi amefiliwa na mzazi-ubeti wa 123)...**hatimizi darahima...**(hafikishi kiwango cha pesa alichohadi – ubeti wa 123)... **hapati hata kituma...** (Hata Mikidadi akichuma mahari kamwe hayapati – ubeti wa 123)...**ataka mtu dhalili...**(anataka mtu masikini, mwenye shida – ubeti wa 130). Jabiri aliwakusanya ndugu zake na kutaka ushauri kutoka kwao. Aliwaambia nduguze kuwa Mayasa aliwakataa matajiri na watu wa kutajika na kumkubali Mikidadi ambaye ni **maskini**. Hii ni kejeli....**ambaye hana nufaa...**(ambaye hana manufaa – ubeti wa 130) Hapa asiyekuwa na manufaa anarejelewa Mikidadi, kwamba hana faida yoyote.

Tazama baadhi ya mifano ya kejeli:

Nduzake wakanena
Mikidadi hi kijana
na kisha kitu hapana
akili haikutua (ubeti wa 131)

Mtuwe ni pepopepo
akili kwake hazipo
na pindi mumuozapo
zitazidi kurufaa (ubeti wa 132)

Katika ubeti wa 131 ndugu zake Jabiri walisema kuwa Mikidadi angali mchanga na akilini mwake hawezi kung'amua jambo yaani ubongoni mwake hamna kitu na pia akili

yake haikutulia. Katika ubeti wa 132 Mikidadi analinganishwa na pepo na asiyekuwa na akili. Hizi zote ni kejeli. Beti za 661, 662 na 663 ni miongoni mwa beti za kukejeli.

3.1.4 CHUKU

Katika tamathali hii, mtunzi hukuza jambo fulani kupita kiasi. Mbinu hii hasa husisitiza ujumbe unaowasilishwa na wala haitumiwi kwa nia mbaya. Mshairi amefaulu katika kutumia mbinu hii pale alipowapa wahusika wake uwezo wa kufanya mambo kinyume na kawaida. Huku tukirejelea utenzi huu, tutazionyesha baadhi ya beti ambapo chuku imetumiwa na pia baadhi ya mishororo katika beti ambapo chuku imetumika vilevile:

Wakangia mbaraza
akamtinda wa kwanza
na wa pili kamsoza
na wa tatu kamtwaa (ubeti wa 278)

na wane hamkamata
na wa tano na wa sita
hisabuye nilopata
khamisini kawondoa (ubeti wa 279)

Katika ubeti wa 278 na 279, Mikidadi alipambana na jeshi katika uwanja wa vita na akafaulu kushinda katika pambano hilo takriban watu hamsini hawakufua dafu, aliweza kuwakabili vilivyo. Mikidadi aliweza kuuwa watu mia moja kwa muda mchache sana (ubeti wa 317). Pia aliweza kuuwa watu mia nne waliokuwa mashujaa (ubeti wa 329). Katika ubeti wa 382 waziri anatumwa alete askari elfu moja ili

wapambane na Mikidadi na Mikidadi anamwambia Sultani kuwa askari alioleta haoni hata mmoja wao kuwa anaweza vita na anamwambia kama ako na wengine awalete (ubeti wa 384). Katika ubeti wa 399, Mikidadi apigwa silaha na askari lakini Mikidadi alizikinga na wala asipate jiraha. Katika ubeti wa 404, Mikidadi anaonekana mwenye furaha na kuwanyang'anya silaha wale askari aliowauwa. Mayasa naye japo ni mwanamke aliweza kupigana na wanaume wengi na kuweza kuwashinda.

Tazama ubeti ufuatao:

Hawale wataka ndoa

ikawa kupinduliwa

Mayasa akiwaua

wengi wakimkimbia (ubeti wa 60)

Lile tukio la Mikidadi kupambanishwa na simba na kupigana naye na kumuua si kitendo cha rahisi hivyo, lakini Mikidadi anafaulu kufanya hivyo na kumkata simba huyo kwa upanga wake (ubeti wa 451). Kwa hakika vitendo vya mashujaa hawa vimekolezwa chuku hata kupita kiasi.

3.1.5 TASHIHISI

Hii ni mbinu ya kukipa kisicho na uhai, sifa za uhai. Mwandishi ametumia tashihisi kwa uchache katika baadhi ya beti: K.m; **ukarudi moyo wake** (ubeti wa 107). Wakati Mikidadi na Mayasa walipopambana ana kwa ana katika mapigano, Mikidadi aliweza kumvua Mayasa taji alilokuwa amelivaa. Kitendo hiki kilimfedhehesha Mayasa kwani hakutaka kuonekana sura zake (ubeti wa 100). Baada ya kuvuliwa taji, Mayasa akaghadhibika sana jambo ambalo lilimfanya Mikidadi apunguze makali yake kivita

dhidi ya Mayasa na moyo wake ukaingiwa na huruma (ukarudi moyo wake) na mahaba ya kumpenda Mayasa. **Roho zao zikajuta** (ubeti wa 318). Yaani lile jeshi la askari baada ya kupigwa na Mikidadi, walibaki kujuta. Nyingine ni: **Kilio kisijifite**, kushindwa kujizuwia ili asilie, (ubeti wa 678), **hata zikija akili**, yaani baada ya ule ulevi kumtoka na kupata akili zake timamu na kuwa razini, (ubeti wa 690) **kwenu kumekukataa**, yaani Mikidadi anamwambia Amiri kuwa, hata kwao hatafikani tena, hana thamani, (ubeti wa 335). **Moyo wake ukarudi**, yaani kuingiwa na huruma, (ubeti wa 193)

3.1.6 DHIHAKA

Katika ubeti wa 227 Luhani anamfanyia Mikidadi dhihaka akimwambia kuwa habari zake anazijua na kwamba alikitaka kuoa na akaktaliwa na mke. Katika ubeti wa 228 Luhani anaendelea kumwambia Mikidadi kuwa Mikidadi alijasiri kuuwa watu, pamoja na masultani kama yeye Luhani, kwa kutaka kuowa akiwa hana chochote kwa hivyo hata asingetamani. Dhihaka hutumiwa kwa lengo la kukera, kuchekesha au kumbeza mtu au hali. Dhihaka alizofanyiwa Mikidadi na Luhani hazikuwa ni za kuchekesha bali ni za kukera na kubeza, kwani Mikidai hakukataliwa na Mayasa wala hakuna mchumba yoyote aliyekataliwa na Mayasa, ila yule aliyeweza kutimiza masharti ya kupigana naye na amshinde ndiye alikuwa awe mchumba wake. Mikidadi mwenyewe alipokuwa wanatoleana historia zao yeye na Amiri, alidai kuwa Jabiri alidhania kwamba kule kuja kumposa mwanawe Mayasa ilikuwa ni dhihaka ndipo akamwandika mali mengi, (ubeti wa 344)

3.1.7 LAKABU

Mtunzi hutumia mbinu hii kuwapa wahusika majina yenye sifa fulani kwa sababu ya tabia fulani ya kipekee. Aidha ni jina la kubandikwa ambalo mhusika hupewa au hata hujipa mwenyewe. Katika utenzi huu kuna wahusika kadha ambao wamepewa au kujipa lakabu wenyewe. ...**Rabi**...(Mwenyezi Mungu – ubeti wa 7, 9 na 695) ...**Jalali**...(Mwenyezi Mungu –ubeti wa 631, 662, 704, 720, 726 na 761)...**Mola**...(Mwenyezi Mungu ubeti wa 8,na 695)...**Jalla wa alla** (Mwenyezi Mungu –ubeti wa 693)...**Jabbari**...(Mwenyezi Mungu –ubeti wa 760 na 769). Mwenyezi Mungu ana majina tisaini na tisa na majina yote haya yana sifa zake nzuri nzuri. Haya tuliyoyataja ni baadhi tu ya majina hayo. Kwa mfano ‘Rabi’ ina maana ‘Bwana’, ‘Jabbari’ ina maana ‘asiyeshindika’. Mtume Muhammad S.A.W. naye pia amepewa lakabu kadha. Miongoni mwa lakabu hizo ni: ...**Mukhtari**...(Mtume Muhammad S.A.W. –ubeti wa 10, 709, 710, 715 na 770)...**Rasuli**...(Mtume Muhammad –ubeti wa 699, 704, 720, 726 na 769). Rasuli ina maana mtu aliyetumwa kwa ajili ya kuongoza watu. ...**Rasua**...(Mtume Muhammad –ubeti wa 767)...**tumwa**...(Mtume Muhammad ikimaanisha mtumishi wa Mungu –ubeti wa 701 na 711)...**Haidari**...(Sayyidina Ali ‘Haidari’ ni utohozi wa jina ‘Haidar’ lililotokana na lahaja ya Kiarabu likiwa na maana ya Simba –ubeti wa 639, 700 na 760). Kulingana na historia ya Kiislamu Sayyidna Ali alikuwa mkali katika vita. Alikuwa ana ujuzi sana wa kuutumia upanga wake uliokuwa na ncha mbili kwa kukatia wapinzani wake. Kwa hivyo sifa hii ya ushujaa imeafikiana sana na lakabu ya ‘Haidari’...**farasi**... (Mikidadi- ubeti wa 294). ... **Simba**... (Mikidadi –ubeti wa 295). Katika beti mbili hizi, Mikidadi anajipa lakabu za farasi na simba. Farasi adui huwa anarusha mateke, anafukuza watu na pia kuuma. Simba pia ni mkali anakula

watu na hata kuogopwa. Mikidadi naye alikuwa ni shujaa, mkali na mwenye moyo wa kupigana.

3.1.8 MAJAZI

Mtunzi amewapa baadhi ya wahusika wake lakabu ambazo zimefanana na sifa zao. Kama tulivyotangulia kutaja katika utangulizi sura ya kwanza, mada ya utenzi huu inataja majina mawili ya wahusika wakuu yaani Mikidadi na Mayasa. Majina haya yametumika kimajazi. Majina Mikidadi na Mayasa asili yake ni kutoka lugha ya Kiarabu. Mikidadi likiwa na maana ya kifaa kinachokata au kuchinja, na Mayasa ni mwanamke mwenye maringo. Kutokana na vitushi vya utenzi huu tunampata Mikidadi akiwaua wapinzani wake wengi kwa kuwakata kwa upanga, kama ianvyothibitika katika baadhi ya beti katika utenzi huu:

Wakangia mbaraza
akamtinda wa kwanza
na wa pili kamsoza
na wa tatu kamtwaa (ubeti wa 278)

kiwakata watu hao
kitwaa silaha zao
na baki wasalio
ni haba walokimbia (ubeti wa 310)

Jina la kimajazi la Mikidadi limelingana sana na tabia yake ile ya kukata wapinzani wake kwa panga katika mapambano yake ya kutafuta mahari ya kumuolea Mayasa.

Jina la Mayasa pia limetumika kimajazi likimaanisha mwanamke mwenye maringo.

Tazama ubeti ufuatao:

Naye Mayasa aringa

maidani kwa upanga

na ambaye ajitenga

akenda hatarejea (ubeti wa 33)

Majazi pia yametumika katika beti zifuatazo: ...**ndimi simba ndimi tui...**(ubeti wa 221)

Katika ubeti huu, zile lakabu alizojipa Mikidadi za simba na chui zimemuafiki, hii ni

kwa sababu wanyama hawa ni mashujaa kama alivyo Mikidadi mwenyewe. Lakabu

alizopewa Sayyidina Ali pia zimetumika kimajazi kama vile **asadi na haidari**. Hivi ni

visawe ambavyo ni vya asili ya Kiarabu vikimaanisha simba kwa lugha ya Kiswahili

ambazo zimesimaia ushujaa.(beti za 631, 639, 700 na 768)

3.2.0 MBINU NYINGINE ZA MATUMIZI YA LUGHA

Mbali na tamathali za usemi kuna na mbinu nyingine za matumizi ya lugha ambazo mtunzi ametumia. Nazo ni tabdila, mazida, usambamba, visawe miongoni mwa nyengine.

3.2.1 TABDILA

Katika mbinu hii mtunzi hubadilisha sauti fulani katika neno kwa lengo la kuleta uwiano fulani, hususan katika kipande cha mwisho cha mshororo. Hili hutokea kwa lengo la kupata kina kifaacho. Baadhi ya maneno yaliyotumiliwa mbinu hii katika utenzi huu ni ...**Mayasi**...(Mayasa- beti za 27, 55,76, 81, 150 na 666). Katika beti hizi nilizozitaja, ilimbidi msanii amalizie na silabi 'si' na wala sio 'sa' kwa madhumuni ya kupata kile kina kinachofaa. Mifano mengine iliyotumiliwa mbinu hii ni:...**anitwale**...(anitwae - ubeti wa 58)...**mashujaani**...(mashujaa-ubeti wa 34)...**hajaribu**...(nikajaribu-ubeti wa 72)...**dhuhi**...(adhuhuri -ubeti wa 85)...**harudi**...(nikarudi-ubeti wa 68)...**amwambile**...(amwambie-ubeti wa 108)...**imzidile**...(ilivyomzidi -ubeti wa 170)...**nufaa**...(manufaa ubeti wa 130)...**hitanga**...(nikitanga -ubeti wa 160)...**khadima**...('khadimu' kwa maana mtumwa -ubeti wa 168)...**hino**..., ...**tupapano**...(hiyo, tupo papa hapa -ubeti wa 322)...**amrukile**...(amrukie -ubeti wa 427)...**yakelea**...(yakwelee -ubeti wa 514)...**shujai**... (shujaa - ubeti wa 366 na 536)...**huyule**...(huyu -ubeti wa 383)...**silahi**... (silaha - ubeti wa 404)...**moleo**...(Mola wako - ubeti wa 555)...**huyuu**...(huyu -ubeti wa 572)...**nduyaa**...('nduyangu' lahaja ya Kiamu ikiwa na maana ndugu yangu -ubeti wa 643)...**tukamuuze**...(tukamuulize -ubeti wa 647)...**kilichotama**...(kilichotamu -ubeti wa 665)...**nimfahama**...(nimfhamu - ubeti wa 706)...**huyuno**...(huyu -ubeti wa 707)...**hama**...(hamu -ubeti wa

724)...**tabasama**...(tabasamu – ubeti wa 724)...**huyunu**... (huyu –ubeti wa 572)...**hawano**... (hao --ubeti wa 555)...**Alia**...(Ali –ubeti wa 729 ,748 na 771)...**Malaka**...(Malaika –ubeti wa 721)

3.2.2 INKISARI

Katika mbinu hii mwandishi hufupisha maneno kwa kupunguza silabi au mizani katika maneno yenyewe kwa lengo la kuleta urafi wa mizani katika mshororo. Mtunzi ametumia inkisari katika beti kadha. Kwa mfano: Katika ub. wa 3, mwandishi ametumia maneno ‘msije ona badala ya ‘musije mukaona’ ‘nawambia’ badala ya ‘ninawaambia’ ‘aibu mkanitia’ badala ya aibu mukanitia’. Kwa kufanya hivi, msanii ameweza kupata mizani zilizo sawa katika kila mshororo wa beti. Inkisari katika utenzi huu imetumika mahli kadha mbali na ubeti huu wa 3: Mifano:...**nami**... (na mimi –ubeti wa 4)...**yu pweke**...(yuko peke yake –ubeti wa 7)...**pekeyo**... , ... **chajiyo** ...(peke yako, cha jioni – ubeti wa 7)...**mtumewe**...(mtume wake –ubeti wa 9)...**ali**...(alikuwa – ubeti wa 13, 18, 19)...**etwa**...(anaitwa –beti za 15 , 43,44,45)...**mjombawe**...(mjomba wake – ubeti wa 16 na 17)...**uzuriwe**...(uzuri wake – ubeti wa 21)...**wakenda**...(wakaenda - ubeti wa 24)...**tamuoa**...(nitamuoa -ubeti wa 24)...**kutaka**..., ...**babaye**...(kukutaka, baba yake-ubeti wa 52)...**fumole**..., ...**ngaoye**...(fomo lenyewe, ngao yenyewe -ubeti wa 57)...**mamboye**, ...**rohoye**...(mambo yenyewe, roho yake -ubeti wa 65)...**nauza**...(nauliza -ubeti wa 69)...**tamshinda**..., ...**tamoua**...(nitamshinda, nitamoua -ubeti wa 72)...**kazidi fanya**...(akazidi kufanya -ubeti wa 77)...**shairile kasha sema**...(shairi lake/lenyewe alipokwisha kulisema -ubeti wa 78)...**warabuo**...(waarabu wako -ubeti wa 126)...**mumuozapo**...(mutakapo kumuozesha -ubeti wa

132)...**vitave**...(vita vyenyewe -ubeti wa 133)...**haibudi**...(haina budi -ubeti wa 140)...**kabaini**...(akabaini -ubeti wa 142)...**tujile**...(tumekuja -ubeti wa 28)...**shoti**...(sharuti - ubeti wa 32)...**naye**...(na yeye -ubeti wa 32, 33, 39)...**jama**...(jamaa - ubeti wa 41)...**mbuzize**...(mbuzi wake - ubeti wa 63)... **isimuyo** ... (isimu yako -ubeti wa 91) ... **kaghadhabu**... (akaghadhibika - ubeti wa 200) ...**akawauza**...(akawauliza -ubeti wa 203)...**hajazo**...(haja zako - ubeti wa 362)...**haibudi**... (haina budi -ubeti wa 499)...**nna**...(ninayo -ubeti wa 519)...**khabarize**...(habari zenyewe -ubeti wa 712)

3.2.3 MAZIDA

Mtunzi ametumia mbinu hii kwa lengo la kutimiza urari wa vina na kusawazisha mizani ya mishororo inayohusika katika shairi. Baadhi ya maneno yaliyorefushwa ni ...**kumuonakwe**...(kumuona -ubeti wa 27)...**mashujaani**...(mashujaa - ubeti wa 34) ...**jeishi**... na **waposhi**... (jeshi na waposi -ubeti wa 45)... **kuwaonake**...(kuwaona - ubeti wa 56)...**mdwara**...(duara -ubeti wa 81)...**bidia**...(bidii -ubeti wa 558) ...**hapano**...(hapa - ubeti wa 476)...**umefikilia**...(umefika -ubeti wa 521)...**huyunu**...(huyu -ubeti wa 572)...**kusikiake**...(kusikia - ubeti wa 642)...**huyule**...(huyu -ubeti wa 100, 175)...**kayafikilia**...(kayafikia -ubeti wa 175)...**kuonake**...(kuona -ubetu wa 182)...**Alii**...(Ali -ubeti wa 723, 730, 732, 733, 734, 738, 741,743, 749, 753 na 770)

3.2.4 TAKRIRI

Hii ni mbinu ya kururudiarudia maneno, sentensi, silabi na mengineyo. Takriri hutumiwa na mshairi kuisisitiza au kushadidia ujumbe ili msomaji apate athari ya msisitizo huo. Katika utenzi huu mshairi ametumia takriri katika viwango tofauti vikiwemo viwango vya irabu, konsonanti, neno na nyinginezo. Baadhi ya takriri zilizotumiwa ni: Takriri maneno:...**sina makini sina**...(ubeti wa 2). Hapa mshairi amerudia neno 'sina' mara mbili. Huu ni msisitizo wa kudhihirisha kwamba hakika amekosa makini. Zifuatazo ni takriri maneno nyengine:...**kabisa kabisa**...(ubeti wa 3)...**hana**...(ubeti wa 8)...**tujile**...(ubeti wa 28)...**mmoja mmoja**...(ubeti wa 42)...**zitungu zitungu**...(ubeti wa 51)...**jaha na jaha**...(ubeti wa 111)...**mumo kwa mumo**...(ubeti wa 113)...**ondokani ondokani**...(ubeti wa 209)...**enendani enendani**...(ubeti wa 307)...**yakwelea**... (ubeti wa 514)...**tena**...(ubeti wa 517)...**kiza**... (ubeti 560)...**endapo**... (ubeti 566)...**taji**...(ubeti wa 588)...**karama 'Illahu karama**... (ubeti wa 590)...**ndimi**...(ubeti wa 599, 600 na 661)...**huna budi huna budi**...(ubeti wa 630)...**jinsi jinsi**... (ubeti wa 666)...**nafusi nafusi**...(ubeti wa 674)...**salamu**...(ubeti wa 708)...**kutwa kutwa**...(ubeti wa 711)...**hana**...(ubeti wa 719)...**enendani enendani**..., ...**upesini upesini**..., ...**mpateni mpateni**...(ubeti wa 722)...**nyumanyuma**...(ubeti wa 733)...**nende**...(ubeti wa 738)

Takriri irabu pia zimetumika na hapa/tuhitajiwa mifano michache tu. Irabu 'a' na 'i' zimerudiwa katika kiambishi 'ali' katika mstari wa kwanza pili na wa tatu ubeti wa 13, pia katika mstari wa kwanza, pili, na wa tatu ubeti wa 335. Lengo la takriri ni kuisisitiza

ujumbe. Mshairi hapa anasistiza juu ya sifa alizokuwa nazo Suwedi za utajiri, mali mengi, msafiri sana, msemi, katili na mwenye akili.

Suwedi ali tajiri

ali na mali kathiri

ali mwingi wa safari

mali akajitumia (ubeti wa 13)

ali msemi wa kweli

ali mwingi wa akili

ali shujaa katili

sultani kamwambia (ubeti wa 355)

Takriri konsonanti pia imetumika mwanzoni mwa sentensi katika baadhi ya beti kwa lengo la mahadhi katika uimbaji shairi. Msomaji anapata ule mpigo wa kishairi. Mfano:

Kawatinda kwa upanga

kwa ghadhabu kumjenga

kawakata kiwatenga

mbali mbali kiwatowa (ubeti 545)

Mtunzi pia ametumia takriri mshororo. Mfano: ...kadiri ulipendalo, kadiri ulipendalo...(beti za 460 na 461). ...akenda akamwegema, akenda akamwegema...(beti za 610 na 610). ...akamwambia Hamza, Hamza akamwambia...(beti za 733 na 734).

Takriri silabi: **matata kukutatia** (ta na ku ubeti wa 634) ni mfano wa takriri silabi

Mikidadi ndugu yangu

takupa wasia wangu

uonapo ulimwengu

matata kukutatia (ubeti wa 334)

3.2.5 UKIUSHI WA KISARUFI

Katika mbinu hii mwandishi hukiuka mpangilio wa sentensi kwa lengo la kusawazisha vina. Kwa mfano:

Nawambia tangu sasa

mambo kabisa kabisa

msije ona makosa

aibu mkanitia (ubeti wa 3)

Ila ana mjombawe

etwa Turadi mtuwe

akenda kukaa naye

mbuzi akimtungia (ubeti wa 16)

Tukirejelea ubeti wa 3, tunapata kwamba ukiushi umetumika katika mshororo wa kwanza na wa nne. Msanii ametumia 'nawambia tangu sasa' badala ya 'tangu sasa nawambia' kwa lengo la kupata kina kinachoishia na 'sa'. Vile vile ametumia 'aibu mkanitia' badala ya 'mkanitia aibu' ili apate ile sauti 'a'. Na katika ubeti wa 16, mshororo wa nne, mwandishi ametumia 'mbuzi akimtungia' badala ya 'akimtungia mbuzi' kwa lengo lile lile la kupata kina kinachoishia na 'a'. Mwandishi asingefanya hivi angekuwa

amekwenda kinyume na ile kaida ya mashairi ya arudhi na ule mpigo wa kishairi ungekosekana. Ukiushi mwengine unadhihirika katika beti zifuatazo: ...**na wa pili mjombawe...**(na mjombawe wa pili –ubeti wa 17)...**hadi mbele akasonga...**(akasonga hadi mbele-ubeti wa 59)...**mayowe kawapigia...**(kawapigia mayowe –ubeti wa 274)...**mkateni chake kitwa...**(kitwa chake mkateni –ubeti wa 288)...**sipeleke tena watu...**(sipeleke watu tena –ubeti wa 312)...**akamfunga na pingu...**(na pingu akamfunga –ubeti wa 335)...**kamwambia Mikidadi...**(Mikidadi kamwambia –ubeti wa 338)...**takujazi mangi mali...**(mali mangi takujazi -ubeti wa 347)...**awanaje mtu huyo...**(mtu huyo awanaje –ubeti wa 353)...**kamwita wake waziri...**(kamwita waziri wake –ubeti wa 354)...**na tamaa umtie...**(na umtie tamaa –ubeti wa 357)...**kamwambia chake kisa...**(kisa chake kamwambia –ubeti wa 373)...**tatwaa silaha zao...**(silaha zao tatwaa –ubeti wa 381)...**nimewana vingi vita...**(vita vingi nimewana –ubeti wa 392)...**umjazi mangi mali...**(umjazi mali mangi –ubeti wa 416)...**nimesafi yangu nia...**(nia yangu nimesafi ama nimesafi nia yangu –ubeti wa 475)...**kwa kutaka lake fungu...**(kwa kutaka fungu lake –ubeti wa 516)...**uyatwae yao mali...**(mali yao uyatwae ama uyatwae mali yao –ubeti wa 553)...**shaka moyo ikatia...**(moyo ikatia shaka –ubeti wa 602)...**waraka kaukutubu...**(kaukutubu waraka –ubeti wa)...**akamwambia Hamza...**(Hamza akamwambia –ubeti wa 734)

3.2.6 TASWIRA

Katika mbinu hii mwandishi huzua picha akilini mwa msomaji kutokana na maelezo yake. Picha hii huwa kama picha halisi kwa msomaji au msikilizaji. Kupitia kwayo

msomaji huhisi, hugusa, hunusa na hata kuona yanayoelezwa. Mwandishi ametumia taswira si haba katika utenzi huu nasi tutatoa mifano mitatu tu:

Akangia kati mwao
kawatawanya wambao
wenye ndoa watakao
kiwakata kiwaua (ubeti wa 86)

Tukirejelea ubeti huo tunaona jinsi Mayasa anavyopigana na waume waliokuja kumposa akiwatawanya na jinsi anavyowakata kwa upanga na akawauwa.

kampigia kwa uti
taji likenda tiati
akamuona binti
suraye kaitambua (ubeti wa 103)

Katika ubeti huo taswira tunayoipata ni ile ya Mikidadi na Mayasa wakiwa vitani na Mikidadi anafaulu kulipiga taji la Mayasa kwa mti wa fumo na taji likamvuka na kuanguka chini na Mikidadi akauona uso wa Mayasa na kumtambua. Taswira ya harufu miongoni mwa nyingine pia inajitokeza. Tazama ubeti ufuatao:

Wakanywa tembo kwa wote
na chakula na mikate
na bangi nayo wavute
wote waele kulewa (ubeti wa 197)

Katika ubeti huu tunapata ile picha ya kunusa harufu ya chakula na vileo vinavyotumiwa vya tembo na bangi. Vyakula, vinywaji kama vile tembo na vinginevyo, na bangi pia huwa na harufu. Kwa hivyo ile taswira ya kunusa humuathiri msomaji na hata ile taswira ya kuhisi njaa na kuwa na hamu ya kula.

3.2.7 MISEMO

Mtunzi ametumia misemo katika utenzi huu kwa kiasi kidogo. Misemo hutilia lugha nakshi na kuifanya ipendeze. Baadhi ya misemo iliyotumika ni: **...nipa takupa...** (nipige nami nikupige –ubeti wa 114). Msemo huu unaashiria kile kitendo cha kupigana baina ya Mikidadi na Mayasa, pale Mayasa alipovuliwa taji lake akakasirika na kuanza kupigana kwa panga. Mayasa akijaribu kumpiga Mikidadi kwa upanga, Mikidadi naye anampiga vile vile kwa upanga wake. Kwa hivyo ikawa ni kile kitendo cha kupigana na kujikinga ili mtu asipate kujeruhiwa. **...hawawezi kumwingia...** (hawawezi kupigana na yeye –ubeti wa 277). Yaani lile jeshi halikuweza kupambana na Mikidadi ambapo lengo lao lilikuwa ni wamkate ama wamkamate. **...mwana mume...** (shujaa –ubeti wa 311). Kile kitendo cha Mikidadi kuweza kuangamiza jeshi lote lile ilibidi wamwambie Sultani kuwa Mikidadi ni ‘mwana mume’ kwa maana ni shujaa.

3.2.8 USAMBAMBA

Huu ni urudiaji wa muundo sawa wa kisintakisia katika virai, kishazi, au sentensi. Kuna usambamba wa kimaana, kidhamira, kisintaksia na aina nyinginezo. Mtunzi (Said Abdalla Masudi) ametumia usambamba wa aina tofauti katika kazi hii, k.v. usambamba wa kimuundo, usambamba wa kitarakimu, usambamba wa kisintaksia miongoni mwa aina nyingine. Zifuatazo ni baadhi ya beti ambazo usambamba umetumiwa: **ndimi simba ndimi tui** (ubeti wa 22). Huu ni usambamba wa kimuundo. Hapa tunapata ruwaza sawa ya kimuundo imerudiwa ‘ndimi’. Yaani ni mimi ‘simba’, ni mimi ‘tui’ kwa maana ya ‘chui’, **ndimi farasi adui, ndimi muondoa dhambi** (ubeti wa 294), Mifano mingine ni: **amtaka amshike, amtwae amteke** (ubeti wa 333), **ni mimi**

muuwa watu, ni mimi simba wa mwitu (ubeti wa 295), kampiga kamtisha, kamshika kamrusha (ubeti wa 334), ndimi simba wa Muungu, ndimi ueka mafungu, ndimi mwana wa makungu... (ubeti wa 599). kampa, kamlabisi (ubeti wa 84), amtaka amjue, yuataka amuo, (ubeti wa 192), ndimi mueka msiba, ndimi mwondoa mahaba, ndimi muweza dharuba (ubeti wa 600), ndimi mvunda buruji, ndimi muondoa miji (ubeti wa 601), mara kwa mara warudi (ubeti wa 608), na wa tano na wa sita (ubeti wa 279). Usambamba huu ni wa kitarakimu. Katika usambamba huu unaofuata, maneno yanaokianzana yametumiwa na mtunzi kwa lengo la kuisitiza: Mfano, za siri na za dhahiri (ubeti wa 490), kwa shimali na yamini (ubeti wa 433)

3.2.9 VISAWAWE

Mbinu hii imetumiwa na mtunzi katika utenzi huu. Visawe hutumiwa kwa minajili ya kuepuka kujirudiarudia. Visawe vimetumiwa katika beti zifuatazo: Mwandishi katika kurejelea majina ya Mwenyezi Mungu ametumia visawe tofauti ambavyo kulingana na dini ya Uislamu, Mwenyezi Mungu ana majina tisaini na tisa ambapo kwa lugha ya Kiarabu huitwa (Asmaul-Husna) yaani majina bora. Majina haya yanasimamia sifa fulani ambazo sifa zenyewe zinamrejelea Mwenyezi Mungu. Baadhi ya majina hayo ni 'Ghafur' yaani mwenye kusamehe dhambi, 'Rahim' mwaenye huruma, miongoni mwa mengine: Mtunzi wa utenzi huu ametumia visawe vifuatavyo kurejelea majina ya Mwenyezi Mungu: ...Rabi...(ubeti wa 7, 9 na 695)...Jalali...(ubeti wa 63, 662, 704, 720, 726 na 761)...Mola...(ubeti wa 8 na 695)...Jalla wa Alla...(ubeti wa 693)...Jabbari...(ubeti wa 760 na 769). Visawe vinavyomrejelea Mtume Muhammad (S.A.W.), ni:...Nabia...(ubeti wa 591)...Nabii...(ubeti wa 770)...Tumwa...(ubeti wa

701 na 711)...**Rasuli**...(ubeti wa 669, 704, 720, 726 na 769)...**Muhtari**...(ubeti wa 10, 709, 710, 715 na 768). Visawe vinavyorejelea vitu vingine ni vile vinavyohusu vita, jeshi, utumwa, na vitu vingine. Haya yanadhihirika katika beti zifuatazo: ...**kondo**... na ...**vita**... na ...**kitali**...(ubeti wa 326 na 543)...**nabaki**... na ...**wasalico**...(ubeti wa 330 na 581)...**jeshi**... na ...**junudi**... (ubeti wa 530)...**mithili** na ...**kama**...(ubeti wa 328)...**wamezie**... na ...**kwisilia**...(ubeti wa 320)...**mume** na ...**rijali**...(ubeti wa 125)...**kukiri**... na ...**kuyakubali**...(ubeti wa 143)...**wangi**... na **akthari**...(ubeti wa 187)...**sakara**... na ...**kulewa**... (ubeti wa 198)...**aseme**... na ...**kamba**...(ubeti wa 219)...**isimu** na ...**jina**...(ubeti wa 257 na 778)...**bidii**... na ...**juhudi**...(ubeti wa 102)...**usiku**... na ...**laili**...(ubeti wa 194)...**mtumwa**... na ...**khadima**... na ...**abidi**...(ubeti wa 168 na 530)...**jini**.. , ...**afriti**... na ...**shaitani**... (ubeti wa 176)...**uzuriwe**... na ...**jamali**...(ubeti wa 21)...**katongoa** na ...**kamba**...(ubeti wa 204)...**ghurushi**... na ...**fulusi** (ubeti wa 229, 230 na 243)...**kitali**... na ... **vita**... (ubeti wa 234 na 235) ...**mithili**... na ..**kama**... (ubeti wa 328 na 485)...**baki**... na ...**wasalico**... (ubeti wa 581) ... **kijana**... na ... **waladi**... (ubeti wa 61)...**kaandika**... na ...**akakutubu**... (ubeti wa 668)...**akatwaa**... na ...**akatukuwa**... ('akatukuwa' ni lahaja ya kiamu ikimaanisha wakachukua –ubeti wa 671)...**ete kauli**... na ...**kamba**...(ubeti wa 510)...**siku**... na ...**ayamu**...(ubeti wa 763)...**furaha**... na ...**sururi**...(ubeti wa 768)

3.2.10 MBINU REJESHI

Mtunzi wa utenzi huu ametumia mbinu hii katika kuwawezesha wahusika wake Mikidadi na wengineo kufafanua mambo ambayo ni mageni kwa wahusika

wengine. Aghalabu hutokea matukio fulani katika kazi za fasihi yakawa ni mageni kwa wasomaji au wasikilizaji ambapo mtunzi akampa nafasi muhusika akayazungumzia na wasomaji nao wakapata kuyaelewa mambo au matukio yenyewe. Baadhi ya beti ambazo mbinu rejeshi imetumika ni:

Alikufa babu yangu
nami nisipate fungu
nimekaa peke yangu
sina kitu kutumia (ubeti wa 259)

Mikidadi kanukuli
niliandikwa mahari
ya Mayasi wa Jabiri
nalimtaka kuoa (ubeti wa 262)

Babaye asikubali
kanandika mangi mali
nami hampa kauli
mahari kumletea (ubeti wa 263)

Katika ubeti wa 259, Mikidadi anaelezea kifo cha baba yake, na hakupata urathi kutoka kwake na alikaa peke yake akiwa hana kitu cha kujikimu nacho katika maisha. Katika ubeti wa 262, anaelezea kuhusu mahari aliyotakikana alipe ili apate kumuowa Mayasa Binti Jabiri na katika ubeti wa 263 anaeleza kukataa kwa babake na ile hila aliyoitumia ya kumlipisha mahari ya kiwango kikubwa naye kuahidi kwamba atatekeleza yote. Katika beti za 341 hadi 344, Amiri anamhadithia Mikidadi

namna alivyopigana na mashujaa wengi, na kuweza kuwashinda kwa urahisi sana. Anaendelea kusema kwamba, alipopambana na Mikidadi hali ilikuwa tofauti na yeye Amiri akaweza kushindwa.

Ndipo pale Amiri anafungwa kwa ukambaa wala si kambaa ambayo ina nguvu zaidi kuliko ukambaa. Hii hapa ni kejeli. Ufahamu wote huu msomaji anaoupata ni kutokana na hii mbinu rejeshi mwandishi alotumia. Vile vile Amiri alimuuliza Mikidadi ile sababu iliyomfanya yeye ahame atoke kwao na kuwaacha ndugu zake na aila yake. Mikidadi naye akamhadithia Amiri kuhusu kumchumbia Mayasa na jinsi baba yake Jabiri alivyomuamulia mahari asiyoweza kuyakidhi. Tazama beti zifuatazo:

kwani mimi si mjinga
mashujaa hiwatinda
sina mwenye kunishiunda
ila kwako sikufaa (ubeti wa 341)

Nambia sababu yako
ilo kukutoa kwako
ukaata nduu zako
Mikidadi kamwambia. (ubeti wa 342)

Akamwambia Amiri
huku kwetu takhubiri
kuna mwana wa Jabiri
nalimtaka kuo (ubeti wa 343)

Nilipokwenda mtaka
Jabiri kamba dhihaka
mali mangi kanandika
yote kamhadithia (ubeti wa 344)

Kwa hivyo Mikidadi hakuwa anajua historia ya Amiri wala Amiri hakujuu ya Mikidadi.

3.2.11 UTOHOZI

Katika mbinu hii mtunzi huchukua neno la lugha fulani na kulipa neno hilo mwendelezo wa lugha pokezi. Lengo la mtunzi kutumia mbinu hii ni kwamba huwa hataki kupoteza maana ya ujumbe uliodhamiriwa au kukosa neno la kutumia katika lugha anayoitumia. Katika utenzi huu, utohozi umetokea katika baadhi ya beti ukiwemo huu wa kwanza: Karibu maneno yote yaliyotoholewa lugha yake pokezi ni ya Kiarabu. Baadhi ya maneno yaliyotoholewa husimamia nomino na baadhi vitenzi na baadhi aina nyengine za maneno. Mfano: ‘akadhukuri’ ni kitenzi na maana yake ni akataja ama akasema (ubeti wa 38), ‘laili’ ni jina likimaanisha usiku (Ubeti wa 194), ‘Khalidi’ ni jina la mtu (ubeti wa 49) Utohozi umetumika katika beti zifuatazo miongoni mwa nyengine: **...awali...**(awal-ubeti wa 1). Awali ni utohozi kutoka neno la Kiarabu ‘awal’ au ‘al awal’ ambapo kwa Kiswahili neno hili maana yake ni mwanzo au kwanza. Mtunzi angetumia neno mwanzo au kwanza, angekosa lile lengo lake la mizani katika mshororo wa ubeti unaohusika. Awali lina mizani tatu na kwanza au mwanzo maneno haya yana mizani mbili kwa kila moja wapo. **...akadhukuri...** (dhakir, ni neno la lugha ya Kiarabu likiwa na maana ya kusema au kutaja -ubeti wa 38). **...kafuria...**(kafuri, ni neno la kiarabu lenye maana ya aina ya manukato, ubeti wa 20)...**bini...**(bin ubeti wa 43)...**khalidi...**(khalid ubeti wa 49)...**rijali...** (rijal –ubeti wa

53)...**shaitani..** (shaitwan -ubeti wa 176). ...**laili...** (lail -ubeti wa 194) ...**khamri...** (khamr -ubeti wa 195)...**waladi...** (walad-ubeti wa 199)...**sahibu...** na ...**taibu...**(swahib na taib ubeti wa 206)...**harabu...**(harab -ubeti wa 215)...**rasi...**(ras -ubeti wa 218)...**jawabu...**(jawab -ubeti wa 233)... **mauti...**(maut -ubeti wa 248) ...**isimu...**(ismu -ubeti wa 257)...**murtadi...**(murtad -ubeti wa 282) ...**junudi...**(junud -ubeti wa 434)...**wahidi...**(wahid -ubeti wa 626)...**Jalali...**(Jalal -ubeti wa 631, 662, 704, 720, 726 na 761)...**Rasuli...**(Rasul -ubeti wa 669, 704, 720, 726 na 769)...**haidari...**(haidar -ubeti wa 638 na 700)...**mukhtari...**(mukhtar -ubeti wa 10, 709, 710, 715 na 768)...**Zakati...**, ... **Saumu...**(Zakat, Swaum -ubeti wa 638)...**halali...**, **haramu...** (halal, haram -ubeti wa 638)... **khabari...** (khabar - ubeti wa 550)

3.2.12 TAHARUKI

Hii ni mbinu ambayo mtunzi hutumia kwa lengo la kumfanya msomaji au msikilizaji wake awe na hamu ya kutaka kung'amua ni kipi kitatendeka kutokana na tukio fulani linaloendelea. Mbinu hii huamsha hisia za msomaji na kuingiwa na hamu na kumfanya kutabiri kile kitakachotokea. Kitendo hiki humfanya msomaji kutaka kusoma zaidi. Baadhi ya beti ambazo mbinu hii imetumika ni pamoja na :

Mjomba wake Turadi
kuona mali kuzidi
kamwambia Mikidadi
umengiwa na kishaa (ubeti wa 155)

Myezi mitatu ikisa

akija mtu kuposa

tutamuoza Mayasa

Mikidadi karidhia (ubeti wa 166)

Katika ubeti wa 155 taharuki inadhihirika kutokana na kauli ya mjomba wake Mikidadi Bwana Turadi kwa kutoamini kuwa kamwe mpwa wake hangeweza kuipata mali yote ile na anaona kama Mikidadi alikuwa ana wazimu. Ubeti wa 166, pale Mikidadi walipowekeana mkataba na Jabiri kuwa miezi mitatu ikiisha kama hajaleta mali waliyoahidiana basi Mayasa aozwe mposi mwengine. Makubaliano haya yaliwaacha wasomaji na ile hamu ya kutaka kujua ikiwa Mikidadi atatimiza ndoto yake au la, huku ikikumbukwa kwamba Mikidadi ni maskini. Ubeti wa 399, mfalme alimwita Mikidadi na akapambanishwa na askari wa mfalme na baada ya wao wawili kuwekeana masharti vita vikaanza na Mikidadi akaibuka mshindi. Hakika mfalme alikuwa na matumaini kuwa angeshinda kwa maana alikubali yale masharti. Katika lile tukio la kupigana na simba (beti za 451 hadi 456), Sultani pamoja na askari na watawala wenzake walikuwa na hamu ya kutaka kujua ni nani atakaye uliwa baina ya simba na Mikidadi. Pia hawakuwa na uhakika kuwa yale aliyoyasema Mikidadi kuwa angeyatimiza au la.

3.2.13 NAHAU

Nahau zimetumika katika beti zifuatazo: **...mali yakatawanyika...**(mali yakachukuliwa na watu yasiyowahusu –ubeti wa 14)...**wakangiana kwa kweli...** (wakapigana kisawasawa –ubeti wa 97) **...wakangiana kwa panga ...** (wakapigana kwa panga -

ubeti wa 105...**babaye keta kauli...**(baba yake kasema -ubeti wa 122)...
atatwondowa...(atatuwa -ubeti wa 435).. **..na nti ikundekunde...**(na masafa
yafupishe -ubeti wa 689)

3.2.14 HITIMISHO

Katika sura hii tumeeleza maana ya tamathali za usemi ni nini pamoja na mbinu nyingine za matumizi ya lugha. Pia tumetaja beti tofauti ambazo tamathali za usemi hizo pamoja na mbinu nyingine za matumizi ya lugha zinapatikana na kuzitolea maana na matumizi yake pamoja na uchanganuzi. Ni matumaini yetu kwamba ufafanuzi wetu ni wa kueleweka na ni wa manufaa kwa kila atakayepitia kazi yetu.

SURA YA NNE

4.0 HITIMISHO

Utangulizi

Katika sura hii ambayo, tutaangazia kwa muhtasari matokeo ya utafiti wetu. Vile vile kutokana na matokeo ya utafiti wetu tutaweza pia kujadili nadharia tete zetu pamoja na kutoa mapendekezo yetu.

4.1 Muhtasari wa maswala muhimu /Muhtasari wa matokeo

Lengo kubwa la utafiti wetu ni kuhusu uchambuzi wa tamathali za usemi pamoja na mbinu nyingine za matumizi ya lugha katika *Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*. Ingawa utenzi huu ni miongoni mwa tenzi za jadi walioshughulikia ni wachache na wengine wao hata hawakushughulikia utenzi huu peke yake bali walikuwa wanalingnisha na tenzi nyingine na walichokishughulikia kilikuwa ni ujumla wa vipengele vya fani zote na wala sio kama sisi ambapo tumeshughulikia viwili tu. Kuna na wengine walioshughulikia utendi huu peke yake lakini mada zao hazikulingana na zetu.

Katika sura ya kwanza, tulianza na utangulizi, tukaelezea swala la utafiti, madhumuni ya utafiti huo pamoja na nadharia tete tulizojikita nazo. Tuliendelea hatua baada ya hatua hadi tukafikia katika ile njia na vigezo tutakavyotumia katika ukusanyaji wetu wa data.

Sura ya pili tulijikita katika kueleza dhana ya fani na tukataja vipengele tofauti vinavyojenga fani na kuvitolea maelezo kwa kuwarejelea maulamaa mbali mbali na pia kuvitolea maelezo yetu.

Baadhi ya vipengele hivyo ni pamoja na lugha, mtindo, ploti, toni, wahusika, mandhari miongoni mwa vyengine. Katika kipengele cha lugha tulielezea ule uhuru ambao mshairi huwa nao katika matumizi yake ya lugha katika ushairi na umuhimu pamoja na ufaafu wake.

Katika sura ya tatu tulijikita na kuzijadili tamathali tofauti tofauti zilizotumika katika utendi huu pamoja na mbinu nyingine za matumizi ya lugha. Tulieleza malengo ya kutumika kwa tamathali pamoja na mbinu nyingine za matumizi ya lugha, tukaeleza maaana na matumizi yazo na pia tukaonyesha beti zilizo na tamathali zenyewe pamoja na mbinu nyingine za matumizi ya lugha. Tuligundua kwamba mtunzi ametumia tamathali za usemi pamoja na mbinu nyingine za matumizi ya lugha nyingi katika kazi yake ijapokuwa nyengine zilitumika kwa uchache sana kama vile nahau na misemo na nyengine hata kutotumika kamwe kama vile methali. Kutumika kwa uchache au kutotumika kabisa kwa baadhii ya tamathali za usemi na mbinu nyingine za matumizi ya lugha, hatutachukulia kwamba ni udhaifu wa mwandishi moja kwa moja kwani pengine hivi ndivyo yeye alivyotaka. Aidha matumizi ya tamthali hizi pamoja na mbinu nyingine za matumizi ya lugha yameboresha na kufanikisha kazi yake mwandishi ya kisanaa na kumwezesha yeye pia kuwasilisha ujumbe aliokusudia.

4.2 Kuhusu nadharia tete

Tulilolishughulikia katika tasnifu hii ni uchambuzi wa tamathali za usemi pamoja na mbinu nyingine za matumizi ya lugha katika *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*. Nadharia tete zetu zilikuwa mbili. Ya kwanza tulichukulia kwamba uteuzi wa tamathali za usemi na mbinu nyingine za matumizi ya lugha katika utendi huu umetekelezwa kwa malengo maalum. Hili limethibitika kuwa kweli na lenye mashiko kwani baadhi ya malengo ya kutumia tamathali za usemi na mbinu nyingine za matumizi ya lugha ni kuleta ule usahali katika kuwasilisha ujumbe au maudhui kwa hadhira.

Usahali huu unamfanya mtunzi atumie mbinu mwafaka ndipo pale mtunzi anapotumia tabdila, inkisari, utohozi, usambamba, tashisi, sitiari, jazanda na tamathali nyinginezo ili kutimiza malengo yake. Nadharia tete ya pili ilihusu uteuzi pamoja na matumizi ya tamathali za usemi pamoja na mbinu nyingine za matumizi ya lugha katika utendi huu umechangia katika ama ufanifu au udhaifu wa kazi hii.

4.3 Mapendekezo

Kazi tuliyoishughulikia sisi imejikita katika kipengele kimojawapo tu cha fani na ambacho ni kidogo (tamathali za usemi) na matumizi mengine ya matumizi ya lugha. Ni matumaini yetu kwamba kutajitokeza na wengine ambao watashughulikia maudhui katika utendi huu au hata walinganishe na tenzi nyingine. Nadharia tuliyotumia ni moja tu, umuundo, ingawaje kazi kama hii pia huweza kutumia nadharia ya Urasimu wa Kirusi.

TULIOWAHOJI

Jina : Ustadh Mahmoud Abdulqadir Mau

Umri: Miaka 70

Makazi: Lamu kisiwani

Tarehe : 19, Julai, 2012

Mada: Maana ya Majina 'Mikidadi' na 'Mayasa'

MAREJELEO

- Abdalla, A. (1973) *Sauti ya Dhiki*. Nairobi: Oxford University Press.
- Abdalla, S.A. (1939) *Al-Inkishafi*. Nairobi: Oxford University Press.
- Abdulaziz, M.H. (1968) 'A note on the form of the language of the poem,' uk.81-83. *The Medicineman* katika Leinhardt, P (mhariri)
- _____ (1979) *Muyaka. 19th Century Swahili Popular Poetry*: Nairobi, Kenya Literature Bureau.
- Abedi, K.A. (1954) *Sheria za kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Dar-es-Salaam: East African Publishing House.
- Allen, J.W.T. (1971) *Tendi*. London: Henemann Publishers.
- Basher, A (1971) *Utendi wa Mikidadi na Mayasa*: Nairobi, Heinema Educational Books (EA) Limited.
- Chiragdin, S. (1987) *Malenga wa Karne Moja*. Nairobi: Longman.
- Faqih, M. (1979) *Utenzi wa Rasi'l Ghuli*, Dar-es-salaam: Tanzania Publishing House.
- Habwe, J/
Karanja, P. (2007) *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Harries, L.H. (1962) *Swahili Poetry*. London: Oxford University Press.
- Kazungu, E.K. (1982) *Deviation and Foregrounding in chosen Swahili Literary Text*, Tasnifu ya M.A., Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Knappert, J. (mhariri) (1964) *Four Swahili Epics*. Leiden: Drukkerij luctor et Emergo.

King'ei, K./

- Amata, K. (2001) *Taaluma ya Ushairi*. Nairobi: Acacia Stantex Publishers.
- Kuvuna, S na wengineo (1992) *Nuru ya Ushairi*. Mwongozo na Uchambuzi: Nairobi, Kenya Literature Bureau.
- Mbatiah, M, (2001) *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.
- Mbayi, L.A. (2009) *Uhakiki wa fani katika tenzi za Howani Mwana Howani Na Mwanakukuwa*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi.(Haijachapishwa)
- Mgullu, R.S. (1999) *Mtalaa wa Isimu.Fonetiki,Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers (K) Ltd.
- Mohamed, S.A. (1980) *Sikate Tamaa*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Msokile, M. (1993) *Misingi ya Uhakiki ya Fasihi*: Nairobi: EAEP.
- Mungai, P.K. (2005) *Uulinganishi wa Kifani wa Tenzi za Mikidadi na Mayasa na Swifa ya Nguvumali*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa)
- Mweri, J.G. (2010) *Utangulizi wa Isimu*: Nairobi, KLB
- Nabhany, A, S. (1987) *Malenga wa Karne Moja*. (Utangulizi). Nairobi: Longman.
- Ndung'o, M./
- Wafula, R. (1993) *Tanzu za Fasihi Simulizi*. BSW 308 (A), Nairobi: University of Nairobi Press
- _____ (1993) *Nadharia ya Fasihi Simulizi*. BSW 308 (B), Nairobi: University of Nairobi Press.
- Njogu. K/
- Chimera, R. (1999) *Ufundishaji wa Fasihi*. Nadharia na Mbinu, Nairobi:Jomo Kenyatta Foundation.

- Wamitila, K.W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi. Misingi na Vipengele Vyake*: Nairobi, Phoenix Publishers.
- _____ (2002) *Kichocheo cha Fasihi. Simulizi na Andishi*: Nairobi, Focus Publishers.
- _____ (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.
- _____ (2008) *Kanzi ya Fasihi I. Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide~ Muwa Publishers Limited.
- Wa Mutiso, K. (1985) *Hurafa na Uyakiniifu Katika Hamziyya*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili: Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- _____ (1996) *Archetypal Motifs in Swahili Islamic Poetry: Kasida Ya Burudai*. Tasnifu ya PhD: Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijachapishwa).
- _____ (2002) *The Epic of Princess Fatuma*. (Mswada).
- _____ (2003) *The Epic of Secrets of All Secrets*. (Mswada).
- _____ (2005) *Utenzi wa Hamziyya*. Dar –es – Salaam: TUKI.